# UTUKUFU

# WA

# MASIHI

*MWANZO WA INJILI YA YESU KRISTO MWANA WA MUNGU*

**MARIKO 1:1**

**PAULO GALLIGAN**
**REVIVAL MINISTRIES AUSTRALIA**

# YALIYOMO

**Ukurasa**

UTANGULIZI ………………………………………………………………………………… 3

MWANZO ……………………………………………………………………………………… 4

INJILI ……………………………………………………………………………………….. 6

YESU ……………………………………………………………………………………………. 9

‘KRISTO’ tafsiri ya MASIHI ……………………………………………………………. 15

MASIHI, YULE MTAWALA MKUU ………………………………………………… 19

YESU WA NAZARETI NDIYE KRISTO ……………………………………………. 23

MWANA WA MUNGU …………………………………………………………………. 28

# UTUKUFU WA MASIHI

## UTANGULIZI

Pengine ufunuo wa muhimu ambao unashuka kanisani siku hizi ni ufunuo wa utukufu wa Masihi. Paulo anatamatisha siri za utajiri wa utukufu wa Mungu katika mataifa kwa maneno mepesi ***"Kristo ndani yenu tumaini la utukufu"*** **(Wakolosai 1:27).** Pole Pole na kwa utaratibu ufunuo huu wa kubadirisha maisha na kubadirisha historia ambayo Petro alikamata kwanza kule Kaisaria Philipi katika **Mathayo 16** unajulikana. Walio na masikio ya kusikia wanaanza kufahamu yakuwa **Kristo ndani Yetu** itakuwa uhakika wa kutembea kwetu. Hili ndilo lengo la huduma ya injili: ***"kwamba Kristo aumbike ndani yetu"*** **(Wagalatia 4:19)**

Petro alisema ***"Wewe ndiwe Masihi [Kristo]"*** **(Mathayo 16:16).**

Masihi ni nani? jina la Masihi ni Yesu, na Yesu ndiye Kristo; Yeye ndiye Masihi. Masihi ni nani? Sehemu kubwa na ya muhimu ya tafakari tutakayotazama katika nakala hii ni kufahamu Umasihi wake, Yakuwa Kristo ndiye mfalme aliyepakwa anayetawala na kutamalaki katika Sayuni.

Tunapofikiri juu ya Yesu Kristo tunamuona tu kama **Mwokozi wetu.** Kwa watu wengi wa Mataifa jina hili 'Masihi' ilikuwa na maana ndogo na kwa wengi haina maana nyingine ila jina la kijamii ya Yesu. Hata hivyo jambo la maana ya imani na la umuhimu kwa kila mmoja kuamini ni hilo.

**YESU NDIYE MASIHI.**

Twapaswa kuhubiri injili ya ufalme wa Mungu na hivyo nilazima pawe na mfalme. Katika siku hizi Mungu ameinua sauti kote katika mwili wa Kristo ambao wameanza kuongea juu ya ufalme wa Mungu. Hata hivyo nilazima tutambue kikamilifu yakuwa:

**Mfalme wa ufalme ni Masihi, Yesu.**

Tumehubiri injili iliyopungukiwa ya wokovu mpaka sasa, tukitazamia sana wokovu kwa njia ya imani ndani ya Yesu kama Mwokozi. Sasa tumeanza kuhubiri injili ya Ufalme wa Mungu, ambao ndio ujumbe [injili] ambayo Mungu ametupatia, kupitia Masihi Yesu, ambayo anaimarisha ufalme Wake hapa duniani kupitia mambalozi wake, Kanisa.

### *"Mwanzo wa injili ya Yesu kristo, Mwana wa Mungu"* Mariko 1:1

Katika aya hii tuna maneno ya muhimu sana tano kama sio sita ambayo kwa pamoja inafanya tangazo la kushangaza kuhusia ambacho hakika tunaamini.

- Neno la kwanza: Ule Mwanzo,
- Neno la pili: ile injili,
- Neno la tatu: Yesu,
- Neno la nne: Masihi [ambayo tafsiri yake ni Masihi]'
- Neno la tano: Mwana wa Mungu, ambalo limeundwa na maneno mawili Mwana na Mungu.

Kufundisha kabisa kutoka aya hii itatusaidia kuelewa injili ya Yesu Kristo yule Masihi, mwana wa Mungu kikamilifu.

# MWANZO

### Mwanzo wa injili ulikuwa upi?

Neno la kwanza ambalo twapaswa kuelewa ni ***"Mwanzo"*** Mwanzo wa injili ni nini? Yesu alikuja katika majira furani akisema ***"Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia; tubuni na kuamini injili."*** **Mariko 1:15.** Huku ndiko kuhubiri kwa kwanza kwa injili. Mazingira yalikuwa yapi na msingi wa Yesu kutokea na kuanza kuhubiri? Kulijibu swali hili kwa wepesi tunatazama mazingira ya **Mariko 1:1-14** za kwanza. Kwa hakika, mazingira makuu ya 'mwanzo wa injili' ni nakala ya Agano la kwanza. Mtume Paulo anatuambia katika **Warumi 1** yakuwa ***"Injili ya Mungu iliahidiwa kwa kinywa cha manabii wake katika maandiko matakatifu"*** **(aya 1b-2)**.

Katika **Mariko 1:1-14,** kuna mambo manne ya mwanzo wa injili:

- Kuhubiri kwa Yohana mbatizaji
- Kubatizwa kwa Yesu na Yohana
- Ushindi dhidi ya shetani
- Yesu alikuja akihubiri injili

### Kuhubiri kwa Yohana mbatizaji.

Katika **Mariko 1** inanukuru kutoka kwa nabii Isaya kumtabuliza Yohana mbatizaji. Mwanzo wa injili ulikuwa na Yohana, mwana wa Zakaraya na Elizabeti. Yohana alikuja akihubiri ubatizo wa toba na ondoleo la dhambi. Huu ndio mwanzo – Nabii yuaja ambaye anajua yakuwa atatanguliza ambaye alinenwa atakuja baada yake; yule aliyekuwako tangu mwanzo. Yohana alikuwa akitangaza mmoja atakayekuja. ***"Yuaja nyuma yangu aliye na nguvu kuliko mimi ambaye mimi sistahili kuinama na kulegeza gidamu za viatu vyake"*** **aya 7.**

Yohana akikuwa amepakwa na Mungu na ujumbe wake ulikuwa wa kugusa sana yakuwa wale wote waliokuwa Judea walikuja kumsikia. Alikuja akihubiri na kubatiza **(aya 4-5).** Yohana alikuja kutimiza maandiko, akitabiri kuja kwake yule aishiye tangia mwanzo, yule wa milele; yakuwa 'Mimi Niko' atakuja kwa mwili. Alikuwa akitangaza yule aliyekuwako tangia mwanzo. ***"Yohana alimshuhudia, akapaza sauti yake akisema, Huyu ndiye niliye nena habari zake yakwamba, Ajaye nyuma yangu amekuwa mbele yangu; kwa maana alikuwa kabla yangu"*** **Yohana 1:15**

### Kubatizwa kwa Yesu na Yohana

Jambo la pili katika mwanzo wa injili ni kubatizwa kwa Yesu na Yohana. ***"Ikawa siku zile, Yesu alikuja kutoka N'azareti ya Galilaya, akabatizwa na Yohana katika Yordani"*** **Mariko 1:9**

**Mathayo 3:13-15** yazungumza juu ya Yesu akija kwa Yohana na kubatizwa. Yesu alimshawishi Yohana yakuwa ni mapenzi ya Mungu yeye abatizwe. Yohana alikuwa na ufunuo huyu alikuwa nani (**Yohana 1:33-34).** Alikuwa amepewa ishara ya kumtambua. Huyu ndiye Yohana alikuwa akihubiri juu yake. Kwa ubatizo waYesu mbingu zilifunguka na Roho wa Mungu akamjia kwa utimilifu (**Mathayo 3:16-17, Mariko 1:10).** Akisha toka kwa maji ya ubatizo, Yesu alipokea Roho bila kipimo na akadhibitishwa kama ***"Mwana".*** Kutoka wakati huo Yesu alikuwa mtu tofauti akitembea na kuhudumu kama mwana.

## Ushindi dhidi ya shetani

Jambo la tatu juu ya mwanzo wa injili ni ushindi dhidi ya shetani. Mara tu baada ya ubatizo Yesu alielekezwa na Roho katika njangwa, ambapo alijaribiwa na shetani (**Mk 1:12-13).** Yesu aliweza kujibu alipopata majaribu katika upeo wa mwili, nafsi na roho, hata kama vile Hawa alivyopata majaribio sawa katika shamba; na Yesu akashinda. Kisha malaika wakaja wakamhudumia (**Mt.4:11).** Yesu kama mwanadamu aliweza kushinda shetani. ***"Yesu akarudi kwa nguvu za roho, akaenda Galilaya; habari zake zikaenea katika nchi zote za kandokando"*** **Lk 4:14.**

## Yesu alikuja akihubiri injili

Jambo la nne katika mwanzo wa injili ni kwamba Yesu alikuja akihubiri injili ya ufalme wa Mungu. Injili ni injili ya ufalme wa Mungu! Kulikuwa na wito wa kutubu na kuamini injili.

Katika kuhubiri injili katika karne iliyopita mkaso ulikuwa ni katika 'mwisho wa injili' hivyo ni Yesu ni mwana wa Mungu na alikufa msalabani kwa sababu ya dhambi zetu; ukiamini hayo utaokolewa. Hata hivyo katika kuhudhurisha injili 'ujumbe uliokamilika' tumeshindwa kushiriki injili kuanzia mwanzo. Mwanafunzi aliyefunzwa vyema ataelewa 'mwanzo wa injili' na ataweza kuwaelekeza watu ***"Kujuwa hakika ya mambo yale uliyofundishwa***" Kwa kutunga kwa taratibu "***habari za mambo yaliyotimizwa katikati yetu, kama walivyotuhadithia wale waliokuwa mashahidi wenye kuyaona, na watumishi wa lile neno tokea mwanzo."*** **Lk 1:1-4**. Katika mwangaza huu mwamini mpya atakuwa amepewa msingi mwema katika elimu ya msingi ya Kristo na hivyo kuwa ameandalika kikamilifu katika kukomaa **(Ebr 6:1-3)**

# INJILI

**Maana ya jina**

Neno la kiyunani 'injili' ni euaggelion SC# 2098; Ina maana 'habari njema' na inatafsiriwa 'Injili'. [mara 46]' Injili ya Kristo [mara 11], Injili ya Mungu {mara 7}, injili ya ufalme [mara 3]

**Asiri ya injili ya pande nyingi (**Haya yote yaliofuata ni kutoka kwa maandiko).

- Mwanzo wa injili (**Mk 1:1, Flp 4:15**)
- Injili ni injili ya ufalme (**Mathayo 4:23**), ni injili ya amani (**Warumi 10:15**)
- Ni injili ya Yesu Kristo (**Mk 1:1**); ni injili ya Mungu (**1 The 2:9, Warumi 1:1**)
- Ni injili ya Masihi (Kristo) (**Rum 1:16**)
- Ni injili ya Mwana wake (**Rum 1:9**); Ni injili ya utukufu wa Masihi (**2 Kor 4:4**)
- Ni injili ya utukufu wa Bwana wa Baraka (**1 Tim 1:11**)
- Injili yastahili kuhubiriwa kwa kila kiumbe (**Mk. 16:15**)
- Ihubiriwe kwa maskini (**Mt 11:5, Lk 4:18**), ihubiriwe hekaluni (**Lk 20:1**)
- Injili ihubiriwe vijiji (**Lk 9:6**), katika vijiji, (**Mdo 8:25**) kwa mji **Mdo 14:21**), katika nchi zilizo mbele (**2 Kor. 10:16**);
- Mungu aliihubiri injili kwa Abrahamu kwanza (**Gal 3:8**)
- Hubiri injili kwa Roho Mtakatifu (**1Pet 1:12**)
- Injili ihubiriwe bila malipo (**1Kor 9:18, 2 Kor 11:7**)
- Ambao wanahubiri injili wanapaswa kuishi kwa injili hiyo (**1Kor 9:14**)
- Tumekabidhiwa injili (**1Kor 9:17**)
- Twatakiwa kuamini injili (**Mk 1:15**) tumeitwa kwa injili (**2Wathesalonike 2:14**)
- Tunapaswa kuitii injili (**Warumi 10:16, 1 petro 4:17**)
- Ukweli wa injili wapaswa kuendelea nasi (**Wakolosai 1:5, Gal. 2:5**)
- Twapaswa kujua siri ya injili (**Efe 6:19**)
- Injili imefichwa kwa wale wanapotea (**2 Kor 4:3**)
- Twapaswa kuhudumu injili (**Kol 1:23**)
- Twapaswa kushuhudia injili ya neema ya Mungu (**Mdo 20:24**)
- Utimilifu wa Baraka wa injili (**Warumi 15:29**)
- Mkishindania imani ya injili (**Flp 1:27**)
- Nikitumika kwa moyo wangu katika injili (**Warumi 1:9**)
- Akitumika kama mwana pamoja nami katika injili (**Wafilipi 2:22**)
- Twapaswa kufanya kazi pamoja katika injili (**Flp 4:3, 1The 3:2**)
- Twapaswa kushiriki katika mateso kwa sababu ya injili (**2 Tim 1:8**)
- Injili ni nguvu za Mungu ziletazo wokovu (**Rum 1:16**)
- Ni injili ya wokovu wetu (**Efe 1:13**)
- Tunazaliwa kupitia nguvu za injili tuwe wana wa Mungu (**1Kor 4:15**)
- Pana ushirika katika injili (**Flp 1:5**)
- Usiondoke kutoka tumaini la injili (**Kol 1:23**)

- Injili kwa waliotahiriwa na kwa wale hawajatahiriwa (**Gal 2:7**)
- Hakuna injili ingine (**2 Kor 11:4, Gal 1:6**)
- Injili isizuiliwe (**Gal 1:7**)
- Ole wangu nisipo ihubiri Injili (**1Kor 9:16**)
- Tumeitwa ili kuitetea na kudhibitisha injili, hata katika minyororo (**Flp 1:7, 17**)
- Uzima na kutokufa zimeletwa kwa nuru kupitia injili (**2 Tim 1:10**)
- Yesu Kristo alifufuliwa kutoka kwa wafu kulingana na injili (**2 Tim 2:8**)
- Hubiria kila taifa, kabila, ndimi na watu injili ya milele (**Ufu 14:6**)

## Injili hii nilazima ihubiriwe

Kuhubiri huku kulianza kwa mahubiri ya Yohana mbatizaji katika jangwa miaka 2000 iliyopita, akijulisha Yesu Masihi. Hii ilikuwa ni kutimizwa kwa unabii wa agano la kale.

Yesu aliamuru mitume ***"Enedeni ulimwenguni kote na kuihubiri injili kwa kila kiumbe"*** **Mk 16:15.** Lile neno 'hubiri 'linamaanisha hubiri injili' Kuhubiri ni kutangaza au matangazo yakuwa Yesu ni Masihi; Yesu ni Bwana. Tunapo yaamini mahubiri kama hayo, kila kitu kinabadirika. Maisha yetu yanaokolewa, yanakombolewa na tunawekwa huru kuishi katika ufalme wa Mungu kwa Roho.

Tumeitwa ***"Kuwahubiria mataifa utajiri wake Kristo usiopimika"*** **(Efe 3:8).** Paulo alikuwa mtume aliyeitwa haswa kwa watu wa mataifa **(Gal 2:8);** Paulo alikuwa **Mwebrania wa Waebrania kwa habari ya kuishika torati, ni farisayo. (Flp 3:6)** alikuwa na uridhi kamili wa kiyahudi kama Wayahudi, kama wayahudi wa siku hizo. Nikupitia uridhi wao kama wayahudi yakwamba Wayahudi wanafahamu Masihi Kristo, ambapo watu wa mataifa hawana uridhi katika Masihi. Waamini kati ya watu wa mataifa wanastahili kufahamu na kuelewa **utajiri wa Kristo usiopimika!**

## Habari njema

'Injili' mwanzo ilijulikana 'dhawabu ya habari njema' lakini baadaye ikaja kujulikana kama habari njema yenyewe. Katika utawala wa Kirumi neno hili lilitajwa kama 'habari njema' juu ya ushindi wa jeshi ingine- habari zilitumwa kwa Rumi kupitia mjumbe yakuwa kulikuwa na ushindi vitani! Kihistoria 'injili'Katika Serekali ya Kirumi ambayo pia iliitwa habari njema juu ya kiongozi akiingia kwa enzi.

Mambo haya mawili ya kihistoria yanatusaidia kufahamu injili ya Yesu Kristo:

- Yeye amejipatia ushindi mkuu, ***"Kwa kusudi hii Mwana wa Mungu alidhihirishwa, ili azivunje kazi za ibilisi"*** **(1 Jhn 3:8b)**
- Amekalia enzi ya Daudi **(Mdo 2:30, 33);** ***"maana sharti amiliki yeye, hata awaweke maadui wake wote chini ya miguu yake"*** (**1Kor 15:25**).

## Yesu alipata ushindi juu ya maadui wake

Injili ni habari njema ama ujumbe wa Yale ambayo Yesu aliye Masihi amekamilisha kupitia kifo chake na kufufuka kwake. ***"Akiisha kuzivua enzi na mamlaka, kuzifanya kuwa mkogo kwa ujasiri, akazishangilia katika msaraba huo"*** **Wakolosai 2:15.** Yaliyotajwa katika aya hii ni kwa kiongozi mwenye ushindi au msimamizi mwenyewe, akirudi Rumi kwa kuushangilia ushindi, wakati ambapo mshindi na kikosi chake walipiga foleni kote kote mitaani, na mateka walioshidwa waliongozwa wakiwa uchi na ilhali wamefungwa minyororo. Huu ndio ubali wa ushindi wa Yesu aliye Masihi juu ya adui. Yesu alileta ushindi kamili juu ya dhambi,

kusimu, kifo na mauti na shetani. Yesu alivua enzi na mamlaka na akazishangilia. Aliweka wazi kushindwa kwa shetani kupitia msaraba. **Hii ndio injili!**

## Dhawabu ni ufalme

Kumbuka injili mwanzo ilimaanisha 'dhawabu ya habari njema'. Kuna dhawabu ya habari njema kwa wale wanaoipokea. Kuna faida kwa wale wanao sikia. Kama habari ikipokelewa kuna dhawabu. Waume na wake watakuja kwa Kristo, Yeye ndiye dhawabu. Kuhubiriwa kwa ufalme wa mbinguni kunaleta wokovu; inahusisha kuleta habari njema ya wokovu. Injili ni injili ya milele yenye dhawabu ya milele. Kwa kuiamini injili tunaingia katika ufalme wa Mungu. ***"Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza ufalme wa mwana wa pendo lake, ambaye katika yeye tuna ukombozi, yaani msamaha wa dhambi"*** **Wakolosai 1:13-14.**

# YESU

## Yesu, kupatikana kwake na kuzaliwa

Yesu ni nani? Yeye ni Yesu wa Nazareti, Aliyezaliwa na Mariamu, aliyepatikana kwa Roho Mtakatifu. ***"Kuzaliwa kwa Yesu kulikuwa hivi: Mariamu mama yake alipokuwa ameposwa na Yusufu, kabla hawajakaribiana alionekana kuwa ana mimba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu"*** **Mat 1:18.** Malaika alikuwa amemwambia Mariamu, ***"Tazama utachukuwa mimba na kuzaa mtoto mwanamume; najina lake utamuita Yesu. Roho Mtakatifu atakujilia juu yako, na nguvu zake aliye juu zitakufunika kama kivuli, kwa sababu hiyo hicho kitakacho zaliwa kitaitwa kitakatifu, Mwana wa Mungu"*** **Lk 1:31, 35.**

Baba yake mlezi alikuwa ni Yusufu na Mungu alimtuma malaika kwa Yusufu akamfunulie asiri ya 'mimba' ya Mariamu ***"Usihofu kumchukua Mariamu mkeo, maana mimba yake ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu"*** **Mt 1:20.** Malaika alimuelekeza Yusufu kuhusu asiri ya Kiungu ya mtoto, yakuwa alikuwa ni kutimizwa kwa unabii wa **Isaya (7:14)** na yakuwa alikua aitwe **YESU.** Yusufu alitii neno la malaika wa Mungu.

## Jina lake na kuwekwa kwake wakfu

Kama ilivyo kuwa katika utamaduni Yesu alitahiriwa na kupewa jina baada ya siku nane na tena alipelekwa katika hekalu kulingana na sheria ***"Zilipo timia siku za kutakasika kwao"*** **Lk 2:21-24**. Wakati mtoto Yesu alipelekwa kwa hekalu 'Simeoni' mtu wa Mungu na mwenye **"haki na mcha Mungu"** na Anna ***"Nabii mke wa miaka themanini na mine"*** wakamtambua Yesu kama Masihi (**Luka 2:25:38)**

## Alizaliwa mfalme wa Wayahudi

Ilikuwa ni baada ya ***"Mamajuzi wa mashariki kufika Yerusalemu kutoka mashariki"*** Wakitafuta mahali alipozaliwa ***"Mfalme wa wayahudi"*** (**Mat 2:1-2).** Yakupendeza kuhani mkuu na waandishi hawakuwa na taabu kutambua yakuwa Masihi [Mfalme] alikuwa azaliwe Bethilehemu. Fahamu kuwa mamajuzi walipata ***"Mtoto pamoja na Mariamu mamaye walipo ingia nyumbani"*** **Mt 2:11**. Tukio la pili katika maisha ya Yesu ilikuwa kutorokea Misri ambapo aliishi na Yusufu na Mariamu hata wakati Mfalme Herode atakapokufa. Yesu akarudi mjini na akaishi Nazareti kama vile malaika alimuelekeza Yusufu.

## Yesu katika umri wa miaka kumi na miwili

Yesu alienda Yerusalemu kwa sikukuu ya pasaka na jamii yake katika umri wa miaka kumi na miwili. Miaka kumi na miwili ilikuwa na maana kubwa kwa kijana Muyahudi na mpaka leo kuna sherehe spesheli katika umri wa miaka kumi na miwili. Sherehe ilionyesha mabadiriko ambayo yanatokea katika maisha ya vijana wanapokua kutoka utoto mpaka mabarehe. Katika tamaduni za wayahudi kuanzia miaka kumi na miwili kijana alikuwa awe na baba yake afundishwe kazi. Wakati Mariamu alimpata Yesu katika hekalu ***"Baada ya siku tatu"*** alisema ***"Baba yako na mimi tulikuwa tukikutafuta kwa huzuni, Akawaambia, kwani kunitafuta? Hamkujua yakua imenipasa kuwamo katika nyumba ya Baba yangu?'"*** **Lk 2:48,49.** Yesu alitafuta kujua mambo ya Baba yake wa mbinguni kwa makini na nilazima iwe alikuwa ameanza kuhisi mabadiriko kwa maisha yake. Hata hivyo alirudi nyumbani nao kwa utiifu **(Lk 2:51)** na tunajua yakuwa alifunzwa kuwa seremala **(Mk. 6:3)**

## Kutimizwa kwa maandiko

Yesu alikuwa ni mbegu ya Daudi ***"Yaani, habari za Mwanawe, aliyezaliwa katika ukoo wa Daudi kwa jinsi ya mwili"*** **Warumi 1:3.** Yesu alikuwa kijana wa kawaida [katika hali] hile ya kukuwa katika kijiji. Babake mlezi alikuwa seremala. Alizaliwa kwa kabila la Yuda. Alikuwa mtu halisi.

Kanisa la Agano la kwanza lilisumbuliwa na wandanganyaji na mpinga Kristo **(2 Yohana 7**). Kuna wale walisema Yesu Kristo hakuja katika Mwili. Niyakimsingi kwa inani ya kweli kuamini na kujua yakuwa Yesu Kristo alikuwa ni Mwanamume halisi, aliyezaliwa na mwanamke; akizaliwa kama mtu wa kawaida [katika mwili] hapa ulimwenguni. Nilazima tukili ***"Yesu kristo yuaja katika mwili"*** **(2 Yohana 7).** Kukili kwingine ni undanganyifu wa mpinga – Kristo. Kuzaliwa kwa Yesu kulikuwa kwa kawaida, kupatikana kwake ilikuwa sio ya kawaida. Malaika alimwambia Yusufu yakwamba kupatikana kwa Yesu kulikuwa ni kutimiza maandiko,

***"Tazama, bikira atachukuwa mimba, Naye atazaa mwana; nao watamwita jina lake Imanueli; yaani Mungu pamoja nasi"*** **Mt 1:23.**

## Jina la Yesu

Jina Yesu, ni la kiyunani, Jesous, ambalo linatamukwa Yay-soos SC#2424. Hii ndio tafsiri ya Kiyunani Yeshua ikimaanisha 'ataokoa' na Yeshua imefupishwa kutoka Yehowshuwa au [Yehowshua] inayotamkwa Yeh-ho-shoo-ah, ambayo inamaanisha Yahweh ni wokovu', YAHWEH ataokoa, au YAHWEH anaokoa.

Maana kamili ya kimsingi ni '*Yahweh ni wokovu'.* Kila mara tunaposema jina la Yesu, tunasema nini? Tunasema, "Yahweh, Mungu wa Agano la kale ambaye alifunua jina lake kwa Musa katika kijiti kwa mwali wa moto, yeye ni wokovu wetu"!

## YESHUA

Wengine wanabishana kwamba Yesu anatakikana wakati wote aitwe kwa jina lake la Kiyunani Yeshua. Wengine wao wanadai yakwamba njina 'YESU ' [Yeshua katika Kiebrania; Yaysoos katika kiyunani; Yesu Katika Myanmar; na pia katika tofauti zingine za lugha] Mungu hakutufanya sisi wote kuwa wanenaji wa Kiebrania na hatarajii tuweze kulinena jina lake kwa Kiebrania. Hata hivyo kuna ufunuo na ufahamu wakupokea kuhusu jina lake tunapo jifunza msingi na chanzo chake.

Kiebrania sio lugha ya agano jipya; bali kiyunani ndiyo lugha ya stakabadthi ambazo zimetufikia. Sehemu ya kujitolea kwetu kwa maandiko nilazima iwe kuzipokea stakabadhi zilizo hifadhiwa.

## Utendaji wa Kimasihi

Wayahudi wengi wanakuja kwa imani ndani ya Yesu aliye Masihi, Mara moja wanamwita Yeshua endapo wananena Kiebrania. Hata hivyo baadhi ya waamini hawa wa Masihi, wanahusisha Watu Wa mataifa ambao wanajitambulisha kama waumini wa Masihi, wanasisitiza yakuwa utafsiri mwingine haufai. Hii haiwezi kutetewa sababu mamilioni yasiohesabika ya waamini wamekuja kwa imani katika Masihi (Kristo) na kumtambua kama Yesu au njina lingine lake kwa lugha zao.

Jambo la kutamka sawa jina lake isiwe kikwazo kati ya waamini wa Masihi na wale ambao wanajiita Wakristo. Mwili wa Yesu kamili ni ***"mtu mmoja mpya kutokana na wawili"*** **(Efe 2:15).** Wayahudi na watu wa mataifa wamepatanishwa ***"Katika mwili mmoja kwa njia ya msalaba, akisha kuufisha ule uadui kwa huo msalaba"*** **(aya 16).** Sehemu ya muhimu ya siri

ya kanisa ni ***“ya kwamba Mataifa ni warithi pamoja nasi wa urithi mmoja, na wa mwili mmoja, na washiriki pamoja nasi wa ahadi yake iliyo katika Kristo Yesu kwa njia ya injili”*** **(Efe 3:6).**

Mimi binafsi nimemjua Yesu zaidi ya miaka 50. Ni hivi juzi nimeanza kuwa na ufahamu wa ndani wa jina lake kutokana na msingi wake katika Kiyunani, na hii imenitajirisha katika kulipokea njina lake ***‘jina lililo juu ya majina yote’*** **(Wafilipi 2:9).** Siri inapo endelea kufunuliwa, hebu tuvumiliane mmoja na mwingine na tusimwekee mwingine vikwaso njiani tukidhania tuna ‘ufahamu wajuu ‘

## JINA LA KIBINAFSI LA MUNGU

Mungu amekuwa Mungu wa kibinafsi na kutoka **Mwanzo 2:4** ***(“YAHWEH Mungu”***) Amekuwa amejulikana kwa jina lake binafsi. Mungu ambaye ni Roho (**Yohana 4:24**) ametuumba katika mfano na sura yake mwenyewe (**Mwanzo 1:26-27**). Katika **Mwanzo 2 kutoka kwa aya 4** Mungu amehusika katika kumuumba mwanadamu na kutayarisha shamba. Anajulikana kama YAHWEH Mungu [kwa Kiebrania YAHWEH Elohim, mara11 katika **Mwanzo 2**]. Mungu alihusika binafsi katika kumuumba mwanadamu na akadhihirishwa kwa mfano ambao sura ya mwanadamu iliumbwa. Mungu alitembea katika shamba (**Mwanzo 3:8**).

### Mungu alidhihirisha jina lake kwa Musa

Katika **Kutoka 3:14 “*Mungu akamuambia Musa, ‘MIMI NIKO AMBAYE NIKO; “akasema ndivyo utakavyo waambia wana wa Israeli; MIMI NIKO [YHWH] amenituma kwenu’’’.*** Jina hili la Mungu halijatafsiriwa katika maandiko ya kingereza. Lakini katika lugha zingine miongoni mwa Kikorea na lugha ya Myanmar, Biblia zao zimetafsiri jina la Mungu katika agano la kale Yehouah (Myanmar) na Yehouavah (Kikorea). Katika lugha hizo mbili tafsiri imefanywa kwa uaminifu katika kutafsiri jina la Mungu kama jina lake binafsi, haswa katika hali fulani.

Jina la kiungu la Mungu, YHWH, inaonekana tu katika Bibilia. Strong’s inatupatia maana kama ‘***Yule aishiye au wa milele’*** na Strong’s yaandika jina kama **Yehovah.**

### Adonai yamaanisha Bwana.

Hata hivyo Biblia ya kingereza imekataa kutafsiri jina la Mungu. Wametafsiri jina la Kiebrania la Mungu BWANA, ambayo sio jina haswa. Jina la Kiebrania la ‘Bwana’ katika agano la kale ni *adonai.* Bwana ni tafsiri zuri ya *adonai.* Yaonekana ya kuwa Wayahudi wa kidini walikuwa wameacha kumuita Mungu kwa jina lake binafsi badala yake walikuwa wakimuita ADONAY, ikimaanisha Bwana. Hii ilifunua kwamba hawakumjua kibinafsi kama akina baba zetu na manabii walivyokuwa wamemjua, hivyo ni, kwa jina lake lililo funuliwa.

### Utamaduni mbaya

Lakuhuzunisha, tafsiri ya Septuagit [agano la kale katika Kiyunani] na tafsiri ya kingereza ziliufuata utamaduni huu [utamaduni usio wa kibiblia]. Watafsiri wa Kiyunani walimuita *kurious* na tafsiri ya Kingereza walimuita BWANA, na Biblia ya Kiswahili ya Afrika ya mashariki wanamuita BWANA, ambayo katika siku za wakoloni ilimaanisha ‘bosi’

### Tetragrammaton/ Uandishi

Jina la Mungu sio BWANA. Jina lake ni Yahweh au Yehovah [Jehovah], ambayo inamaanisha “MIMI NDIYE”. Helufi za Kiebrania YHWH ya jina inaitwa tetragrammaton /ni

uandishi; Hakuna matamshi kama hayo, ambayo ni vingumu kutamka. Hata hivyo hii si sababu tosha ya kubadirisha tafsiri kabisa.

Utamaduni uliotafsiri ulifuata msingi wa tabia za kiyahudi kutoka zamani. Ni wao walioanza tabia za kumuita Mungu, Bwana, kwa kutumia uandishi ulioongezea matamshi, hivyo ni jina *adonay.* Katika Kiebrania halisi jina hili halina matamshi wala sauti. Kwa hivyo siojambo lisilo la kawaida kuuchukua mweelekeo huo wa Jina lililodhihirishwa la Mungu. Wakati wowote ambapo ***"Mwanafunzi wa kiyahudi anatazama Uandishi [wakilitaja jina la Bwana] wanalisoma adonay"*** Watafsiri wa Kiyunani na Kingereza walichukua tabia hiyo.

## Ufunuo wa ndani wa jina hilo.

Wengi wametatanikiwa kwa sababu ya maandiko katika **Kutoka 6:2-3** wakati Mungu alisema na Musa ***"Kisha Mungu akasema na Musa, akamwambia, Mimi ni Yehovah; nami nilimtokea Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo kama Mungu mwenyezi, bali kwa jina langu YEHOVAH sikujulikana"*** Hii ni kumaanisha ya kwamba Mungu hakujulikana na baba zetu kwa jina lake? Sio hivyo, nakara ya maandiko ni wazi: Adamu na mkewe walimjua Mungu kwa jina lake binafsi, lakini baba zetu hawakufahamu maelezo kamili na kulipokea jina hilo lililo dhihirishwa ambalo lingeleta ukombozi kwa taifa lote kwa wazao wao kwa mamia ya miaka.

***"Waambie wana wa Israeli maneno haya, BWANA (YHWH) Mungu wa baba zenu, Mungu wa Ibrahimu, Mungu wa Isaka, Mungu wa Yakobo, amenituma kwenu; hili ndilo jina langu hata milele, nalo ni kumbukumbu hata milele."*** **Kutoka 3:15**. Wakati Mungu kwanza alidhihirisha jina lake kwa Musa ilikuwa ni ili wazee katika Misri wampokee Musa wakati alikuja kwa jina ambalo wazee walilo mjua kwalo.

***"Eneda ukawakusanye wazee wa Israeli pamoja, ukawaambie, BWANA(YHWH) Mungu wa baba zenu, Mungu wa Ibrahimu, Mungu wa Isaaka, Mungu wa Yakobo, amenitokea, akaniambia, Hakika nimewajilieni, tena nimeyaona mnayotendewa huko Misri; Nami nimesema, Nitawapandisha kutoka katika mateso ya Misri na kuwaingiza katika nchi" Kutoka 3:16-17.*** Wazee wa Israeli walijua jina la Mungu lakini kama baba zao Ibrahimu, Isaka na Yakobo, hawakujua ufunuo wa jina ambalo Musa alilokuwa amewaletea.

## MIMI NIKO ina maana gani?

- Inamaanisha Yeye ni kila kitu ambacho kiko;
- Inamaanisha Yeye ndiye wa milele;
- Inamaanisha Yeye ndiye ajidumishaye;
- Inamaanisha Yeye ndiye uzima ;
- Inamaanisha Yeye ndiye nuru;
- Inamaanisha Yeye ndiye Muumbaji;
- Yeye ndiye kila kitu.

Wakati Mungu anasema "MIMI NIKO" Inamaanisha **Yeye yuko.** Hakuna kitu kinakosekana ndani ya Mungu; hakuna cha ziada cha kufanyika ndani ya Mungu, ambacho hakiko ndani ya Mungu. Hakuna kitu ndani ya Mungu ambacho hakistahili kuwa ndani ya Mungu. Yeye ni Mungu na anajidhihirisha kama **"**MIMI NIKO**"**.

***"MIMI NIKO, kabla yangu hakuumbwa Mungu awaye yote, wala baada Yangu mimi hatakuwako mwingine"*** **Isaya 43:10**.

### Jina lake ni ajabu.

Wakati Manoa, babake Samsoni, alimuuliza malaika wa Yehovah, ***"Jina lako ni nani"?*** Alijibu akasema, ***"Mbona waniuliza jina Langu, ukiona kuwa ni ajabu?"*** (**Waamuzi. 13:17-18)** Jina la Mungu ni ajabu. Isaya alitabiri juu ya Masihi, **"*Naye ataitwa jina lake, Mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani"*** **Isaya 9:6.** Isaya anajumuisha majina haya yote kwa Masihi, Yesu, haya ni yaajabu jinsi gani!

### Jina , *Ha Shem* [Kiebrania Kwa jina] haijatafsiriwa

Jina lililofunuliwa la Mungu limetumika zaidi ya mara 6,500. Kwa hivyo kwa zaidi ya mara 6,500 hili jina BWANA limetumika na helufi kubwa nne likionyesha jina la Mungu.

Kwa kukosa tafsiri ya jina la kibinafsi la Mungu katika agano la kale katika biblia ya Kingereza, ikifuatwa na kutofahamu kwa jina la Yesu katika agano jipya, hatujahisi ya kuwa jina la Yesu lina nguvu sana hata kama tumejua yakuwa jina Lake lina nguvu. Lakini sasa tunaendelea kufahamu: Ni jina la Yahweh; ni jina lililodhihirishwa la Mungu. Jina la Mungu halija badirika.

Ni kwa kutofahamu Jina la Yesu kuna kutatanikiwa kwingi kuhusu tabia wazi za kiutume katika kitabu cha Matendo kubatiza katika Jina la ***"Yesu Kristo"*** **(Act 2:38)** ***au jina la Bwana Yesu"*** (**Mdo 8: 16; 19:5**). Katika kuyatimiza alioamuru katika **Mathayo 28:19** ***"Mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu"***

### Kutoka Agano la kale hadi Jipya

Jina la Mungu, Jina lake binafsi, ni la muhimu sana. Tunalifahamu jina la Bwana katika agano jipya ni jina la Yesu, au jina lililolingana na hilo katika kila lugha. Yesu ameitanishwa na Baba, jina Yahweh la Agano la Kale. Kwa hivyo andiko lisemalo ***"Mungu alimwadhimisha mno,*** (Kunena juu ya Yesu) ***akamkirimia Jina lile lipitalo kila jina; Ili kwa jina la Yesu"*** (**Wafilipi 2:9 -10a**), inaanza kufanya mabadiriko yenye maana.

Ingekuwa aje jina la Yesu liwe juu ya jina la Yehovah wa agano la kale? Ilikuwa, Haingekuwa. Kwa sababu **Jina la Yesu ni jina la Yahweh,** kwa hivyo inaleta maana. Ni kwa hakika ***"Mungu alikuwa ndani ya Kristo"*** **(2 Kor 5:19),** na katika Kristo Yesu Bwana wetu ***"unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili"*** **(Wakorosai 2:9),** Kwamba tunakuja kufahamu yakuwa jina la Yesu ni jina la Mungu; kwamba Mungu anawakirishwa kikamilifu na kudhihirishwa katika jina hilo.

**Yohana 1:14** inasema ***"Naye neno akafanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli"*** Huyo Neno ***"Mwanzo alikuwako kwa Mungu"*** **aya 2** ***"Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu*** *[Hii inatoka moja kwa moja kwa kiyunani]"* Na jina lake ni lipi? Yeshua au Yesu, na Yeshua inamaanisha nini – Yahweh ni wokovu wetu. Mungu wa agano la kale alifanyika mwili na akaishi miongoni mwetu!

- **Hii ni siri ya utauwa! 1 Tim 3: 16.**

### YESU NDIYE 'MIMI NIKO'

Yesu alijitambulisha kama 'MIMI NIKO' katika **Yohana 8:58** ***"Yesu akamwabia, Amin, amin, nawaabia, Yeye Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO."*** Tena katika **Yohana 18:5,** wakati walikuja kumkamata Yesu akawauliza wanamtafuta nani, ***"Wao wakajibu, Ni Yesu mnazareti. Yesu akawaambia 'MIMI NIKO'"***. Basi alipo waambia MIMI NIKO, walirudi nyuma, wakaanguka chini (**aya 6**).

**Katika injili ya Yohana kuna misemo saba ya "Mimi ndiye:**

i. Mimi ndimi chakula cha uzima **(6:35)**
ii. Mimi ni nuru ya ulimwengu **(9:5)**
iii. Mimi ndimi mlango wa kondoo **(10:7)**
iv. Mimi ndimi mchungaji mwema **(10:11)**
v. Mimi ndimi huo ufufuo **(11:25)**
vi. Mimi ndimi njia, na kweli na uzima **(14:6)**
vii. Mimi ndimi mzabibu wa kweli **(15:1)**

Misemo hii yote inaeleza wazi: Matumizi ya ukweli ya jina la Yahweh ikionyesha yakuwa Yesu ni jina la MUNGU, kikamilifu na kamili.

## Yesu ndiye Mwokozi

Katika agano jipya Yesu anaitwa Mwokozi (**Luka 2:11**). Mwokozi ndilo jina la Yesu – Yahweh ni wokovu. Malaika alimwambia Yusufu, ***"Nawe utamuita jina lake Yesu, maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao"*** **(Mat.1:21),** na malaika akawaambia wachungaji, ***"Maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa, kwa ajili yenu, Mwokozi, ndiye Kristo Bwana"*** **Luka 2:11.** Yesu ndiye Mwokozi. Wokovu ambao Yesu analeta unaonyeshwa katika jina alilopewa.

Jina lile kwa kiyunani linamaanisha mkombozi. Katika Agano Jipya la Kiyahudi hilo neno limetafsiriwa mkombozi, badala ya mwokozi, tofauti ya majina haya mawili ni ipi?

Kimsingi hakuna tofauti, lakini Mkombozi anaweza kuwa na nguvu, ikionyesha kitu chenye uweza kinatendeka.

Yesu mkombozi wetu atawashinda adui zetu. Atatukomboa kutokana na shida. Atatuinua katika uhuru, nje na utumwa. Yeye ni Mkombozi! Jina mwokozi linamaana ile, lakini tumelifanya jina lile kuwa nila kidini sana

## Joo uone!

***"Filipo akamwona Nathanaeli, akamwambia, Tumemuona yeye aliye andikiwa na Musa katika torati na manabii, Yesu mwana wa Yusufu mtu wa Nazareti, Nathanieli akamwambia, laweza neno njema kutoka Nazareti? Filipo akamwambia Joo uone"*** **John 1:45-46.** Wakati Nathanieli alipotoka kumlaki Yesu na kumtambua kwa Roho mara moja tu Nathanieli alitangaza, ***"Rabi, wewe u Mwana wa Mungu, ndiwe mfalme wa Israeli"*** **(aya 49)**

Baada ya Yesu kunena na yule mwanamke kwenye kisima kuhusu maisha yake ya ndani na kuhusu asiri ya ibada ya kweli, alisema kwake, ***"Najuwa ya kuwa yuaja Masihi aitwaye (Kristo); naye atakapo kuja, yeye atatufunulia mambo yote".*** Kisha Yesu akamwambia, ***"Mimi ninayesema nawe ndiye,"*** **(Yohana 4:25-26).** Kwa kweli, ***'MIMI NIKO ninayezungumza nawe.'***

**Twahitaji ufunuo wa Yesu Ni nani!**

# ‘KRISTO’ tafsiri ya MASIHI

Katika **Mathayo 16** Yesu aliwapeleka wanafunzi wake ***“Kaisaria – Philipi”***, **(aya 13).** Huu ulikuwa ni mji wa watu wa Mataifa lakini ni hapa ambapo ufunuo wa kukubukwa ulipatiwa Petro. ***“Yesu akauliza wanafunzi wake akasema ‘Watu hunena kuwa mwana wa Adamu kuwa ni nani?*** Wanafunzi walimpa jibu tofauti tofauti nakisha akauliza ***“Nanyi mwaninena mimi kuwa ni nani?*** **Aya 15** ***“Simioni Petro akajibu akasema, Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai”*** **(aya 16)** Ni katika msingi wa ufunuo huu ambapo Yesu alisema atalijenga kanisa lake.

## MASIHI NI NANI?

Ufunuo wa kufungua wa Petro ***“Wewe ndiwe Masihi Mwana wa Mungu aliye hai”*** **(Mat 16:16)** ulikuwa ni wimbo kwa masikio ya Yesu. Alisema katika Mwamba huu wa ufunuo ***“Nitalijenga kanisa langu’*** **(aya 18)**. Ufunuo alioupata Petro ni upi? Katika biblia zetu za kingereza na karibu tafsiri zote za lugha za Mataifa, tunamuita Yesu ‘Kristo’, ambayo msingi wake ni katika jina la Kiyunani *christos* – ambalo limetafsiriwa moja kwa moja kutoka Kiebrania neno *Meshiyach*– na hatuna ufahamu wowote wa jina ‘Kristo’.

Biblia nyingi za Mataifa zimetafsiri ‘*Messiah’* kama ‘*Kristo.’* Wakati jina hili kimsingi lina maana sawa na neno la kimsingi la Kiebrania ‘*Messiah’,* Kutambuliwa kwa Yesu kama Kristo hakuna maana yoyote kwa mawazo ya wakristo wa Mataifa. Biblia ya kingereza ya Kiyahudi, Agano Jipya, haitumii jina ‘*Kristo’* lakini wanamuita Yesu ‘*Messiah’* na kwa jumla Wayahudi ambao wanamuamini Yesu wameunda vikundi vya Kimasihi, na hawataki kujiunga na makanisa ya wakristo wa Kimataifa. Hii inatokana na tabia za kuwapinga Wayahudi na tabia za baadhi ya makanisa ya wakristo wa kimataifa kwa karne nyingi. Hata hivyo swala la ndani ni jambo la kutofahamu miongoni mwa waamini wa Mataifa kuhusu ***“Kristo ni nani?”***

## KRISTO

‘Christ’ Strong’s Concordance {SC#} 5547 Gr. ‘Christos’ kutoka #5548 kupaka, au kusugua kwa mafuta, mfano, kumtenga mtu kwa ofisi au huduma za kidini. Imetafsiriwa aliyepakwa Christos inamaanisha aliyepakwa, Masihi … Kumekuwa na shinda katika kanisa la Mataifa ya kutoelewa ‘Yesu’ ni nani. Kristo limekuwa Jina la kumueleza Yesu tu, **Sio ufunuo wa kujuwa Yesu ni nani!**

## MASIHI

‘*Messiah’* SC# 499 Hb. *Mashiyach* kutoka #4886 Kusugua kwa mafuta, kupaka (kutenga) ‘*Mashiyachi’* inamaanisha kupaka, kumtenga mtu kwa ofisi [kuhani au mfalme], haswa *Masihi,* iliyotafsiriwa aliyepakwa, *Masihi*. Masihi imetumika mara mbili tu katika Biblia ya mfalme Yakobo katika Agano la Kale, na mara mbili katika Agano Jipya, neno la Kiebrania lililobebwa.

Kristo inazungumzia Mesiah [aliyepakwa]. Kulingana na Strong’s Jina hili Kristo ni la kumueleza Yesu, hivyo ni, neno la kingereza kumaanisha neno la kuelezea mtu.’ Neno ‘Kristo’ likiwa linaelezea hutusaidia kufahamu Yesu ni nani. Lakini haina maana kubwa. Kwa hivyo Kristo inamaanisha nini? Nikwa nini tunamuita mwana wa Mungu, Yesu Kristo? Kwa wengine ni jina la kijamii. Pengine jina la Baba yake lilikuwa ni Kristo?

Yesu Kristo? Tumemjuwa Yeye kama Mwokozi wetu, na hatujajihusisha juu ya maana ya 'Kristo'. Jina Kristo linapatikana zaidi ya mara 550 katika Agano Jipya. Kuna umuhimu uliotiwa mkaso katika Agano Jipya katika uhakika wa kuwa Yesu ndiye Masihi. Kusudi la Agano Jipya ni kudhihirisha kwa kila Mtu yakuwa Yesu ndiye Masihi [Kristo] Hivyo ndiyo Jambo kubwa la Agano Jipya.

### Masihi ndiye Mfalme aliyeahidiwa, yule mkombozi

Neno Masihi limetafsiriwa, Kristo katika tafsiri nyingi za Biblia za watu wa Mataifa' Aliyetumwa 'Aliyepakwa', lakini pia inazungumza juu ya mwana mkuu wa Daudi aliyeahidiwa (**2 Samueli 7:12-14,16**) atakayeketi katika enzi ya Daudi na kutawala milele; **Kwa hivyo Masihi ndiye Mfalme aliyeahidiwa atakaye wakomboa watu wa Mungu kutoka kwa maadui wake wote.** Katika Agano Jipya la wayahudi, neno 'Mwokozi' limetafsiriwa 'Mkombozi'. Maneno hayo yote mawili yamekubalika lakini ninataka tuanze kuelewa maana yenye nguvu zaidi [hata ya kijeshi] asiri ya matarajio ya kihistoria ya Masihi: Angekuwa ni mkombozi mkuu!

### Ufunuo wa ndani wa kristo

Ni ya muhimu tusome tena Agano la Kale tukiweka jina 'Masihi' badala ya Kristo', au tufahamu yakuwa tunaposoma neno 'Kristo' maadiko yanaongea juu ya Mfalme mkuu aliyetarajiwa kuja na Mfalme huyo ni Yesu.

### Yeye ana mamlaka yote

Masihi inamaanisha mwana wa Daudi wa ahadi atakayeketi kwenye enzi [Sasa Sayuni ya mbinguni] na kutawala na kutamalaki kutoka wakati huo. Mfalme huyu [Masihi] atakuwa na mamlaka yote na nguvu zote na Yesu alionyesha kuwa na mamlaka hayo; alisema ***"Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani"*** **(Mt 28:18)** Wakati kanisa linakuja kufahamu cheo na ofisi ya Kristo, hapo tutatembea katika upeo mkuu wa mamlaka na ushindi kama Kanisa lake.

### Ameinuliwa katika Mkono wa kuume

Yesu amekuwa amekalia enzi na akitawala kama Masihi tangu alipopaa. Petro alitangaza yakwamba thihirisho yakwamba Yesu ***"ameinuliwa katika mkono wa kuume wa Mungu"*** ilikuwa ni kuthihirishwa kwa kumwagwa kwa Roho Mtakatifu siku ya pentekote ***"Basi yeye, akiisha kupandishwa hata mkono wa kuume wa Mungu, na kupokea kwa Baba ile ahadi ya Roho Mtakatifu, amekimwaga kitu hiki mnacho kiona sasa na kukisikia*** **(Mdo 2:33)**

### Uweza wa kifalme utaongezeka

Isaya alitangaza yakuwa mara tu atakapoinuliwa juu ya enzi, uweza wa Kifalme utaongezeka kuanzia wakati huo. ***"Maongeo ya enzi yake na amani hayatakuwa na mwisho kamwe. Katika kiti cha enzi cha Daudi na ufalme wake; kuuthibitisha na kuutegemeza kwa hukumu na kwa haki, Tangu sasa hata milele. Wivu wa BWANA (Yahweh) wa majeshi ndio utakaotenda hayo"*** **Isaya 9:7.**

### Anatutuma kwa Mataifa

Ni huyu Kristo aliye na mamlaka yote mbinguni na duniani (**Mathaya 28:18)** aliye tutuma kama mitume na kanisa la kitume kwa watu wa mataifa kuwafanya wanafunzi, tukiwabatiza katika jina lililo funuliwa la Baba Mwana na Roho Mtakatifu, ambalo ni jina la Yesu, na kuwafundisha kuyashika yote ya Yesu. **(Mt 28: 19-20)**

## Tunaomba na mamlaka makuu

Tunapo pokea ufunuo huu wa Yesu ni nani', ufahamu wetu wa injili unaongezeka na maisha yetu ya maombi yanabadirika. Hii ni kwa sababu tutaomba na mamlaka kamili kama mabalozi tukiwakilisha Serikali ya Mungu na tukiwa tumepokea mamlaka ya ufalme wa mbinguni. Zaidi ya mara 550 tumeonyeshwa Masihi [Kristo] na maandiko inatangaza yuko ndani yetu. Je hiyo ni ajabu kuu namna gani! ***"Kristo ndani yetu tumaini la utukufu"*** **(Wakolosai 1:27).**

## Kudhibitisha yakuwa Yesu ndiye Masihi

Ina maana gani kusema Yesu, ***"wewe ndiwe Masihi"?*** katika **Mathayo 16:16,** Ufunuo wa Petro ulikuwa kwamba alimtambua Yesu. Alisema "Wewe ndiwe Masihi, Mwana wa Mungu aishiye milele." Masihi ni Yesu; Yesu ndiye Kristo, ndiye Masihi. Kristo na Masihi zinamaanisha kitu kimoja.

Kila mara tunapofikiria juu ya Yesu Kristo, tunamfikiria kama mwokozi wetu, hata hivyo jambo la imani lililo la muhimu kwetu ni kuamini ya kuwa Yesu ni Masihi. Jambo kamili ya Mahubiri ya Petro katika siku ya pentekote, ni katika kumwagwa kwa Roho Mtakatifu na kutatanikiwa kwa umati uliokusanyika mitaani, ilikuwa kuwadhibitishia kutoka maandiko katika Agano la Kale yakuwa Yesu wa Nazareti, aliyesulibishwa, alikuwa hakika ndiye Masihi **(Mdo 2:17-36)**

Katika **Mdo 5:42** ufufuo ulipoendelea Yerusalemu katika mwamko wa kuja kwake Roho Mtakatifu, Biblia inasema, Ikizungumza juu ya mitume napengine wanafunzi wengine kwa wakati huu, ***"Na kila siku, ndani ya hekalu na nyumbani mwao, hawakuacha kufundisha na kuhubiri habari njema za Yesu kuwa ni Kristo. [Masihi]"***

## Kwanza kwa Wayahudi

Katika huduma ya kanisa la kwanza, hawakukoma kufundisha na kuhubiri yakwamba Yesu wa Nazareti ndiye Masihi. Walifanya hivyo katika hekalu, walifanya hivyo kwa nyumba. Kwa njia nyingine walifanya hivyo kwa hadhara na katika nyumba. Ujumbe wao ulikuwa upi? Walikuwa wakidhibitisha kutoka maandiko ya Agano la Kale yakuwa Yesu wa Nazareti ndiye Masihi. Mahubiri hayo yalikuwa na maana kubwa kwa wale waliohubiriwa; walikuwa wakiwahubiria wayahudi katika Yerusalemu!

## Kwa watu wa mataifa

Injili ilitanda kwa Mataifa: Petro alihubiri katika nyumba ya Kornelio **(Mdo 10)** na baadhi ya wanafunzi waliinua kanisa katika Antiokia ikihusisha Wayunani na Wayahudi (**Mdo 11).** Paulo aliinuliwa kama mtume kwa Mataifa **(Gal 2:8).** Kuhubiri Kristo ilikuwa sasa kwa Mataifa. Paulo alipewa neema ya ***"Kuwahubiria mataifa utajiri wake Kristo usiopimika"*** **(Eph 3:8)**

Kwa wayahudi ujumbe mkuu ulikuwa kujuwa kwamba Yesu wa Nazareti waliyemsulibisha alikuwa ndiye Masihi. Hata hivyo Mataifa walikuwa wanaufahamu mdogo wa Masihi na kwa hivyo mzigo wa ujumbe ulikuwa ni Kristo kwao. Wayahudi walielewa mambo mengi ya Masihi na walikuwa na matarajio ya kuja kwake; Mataifa walijuwa kidogo au hawakujuwa juu ya Masihi na walihitaji maelezo kamili juu ya Masihi ni nani na kuwa Yesu ni Masihi.

### Wayahudi na Mataifa pamoja ndani ya Masihi

Kanisa lilianza na kuwahubiria Wayahudi Yerusalemu na Judea kisha ikatanda hadi Samaria. Hatua nyingine kuu ilikuwa ni katika Antiokia ya Siria. Ni nini kilikuwa cha ajabu kule Antiokia? Wayahudi na Mataifa walikuwa wanaabudu pamoja. Hii ilikuwa ni hatua ya ziada kwa kuimarishwa kwa kanisa la kweli, sio kanisa la Wayahudi peke yao kama pale Yerusalemu, wala kanisa la Mataifa kama vile yameinuka katika historia lakini ni mwili wa Yesu ikijengwa na Wayahudi na Mataifa pamoja. Sasa katika nyakati hizi za mwisho tunatazamia Mungu kuwaleta Wayahudi na Mataifa pamoja tena katika mwili wa Kristo, wakiabudu pamoja kama mtu mmoja mpya

Katika **Warumi 11,** Paulo anaongea juu ya anguko la wengi la Wayahudi ambao hawakumkubali Yesu kama Masihi katika karne ya kwanza. Wakati huo ***"yako mabaki waliochaguliwa kwa neema"*** waliokolewa **(aya 5).** Kupitia kuanguka kwa Wayahudi, ***"Wokovu umewafikia Mataifa, ili wao wenyewe watiwe wivu"*** **(aya 11)**. Hata hivyo katika historia, kanisa la kikristo lilianguka na likapotoka; miongoni mwa hayo ikiwa ni kuwatesa Wayahudi. Sasa katika nyakati za mwisho, Yesu aliye kichwa cha kanisa, analirejesha kanisa lake na kuliandaa kanisa lake liwe Bibi harusi mwenye utukufu (**Efe 5:26-27**). Kanisa hili ni ushirika wa waridhi pamoja: Wayahudi na watu wa Mataifa **(Efe 3:6, & 2:14-16)**, Na kanisa la mwisho ambalo litainuka litakuwa ni ushirika mkamilifu wa Kimasihi Wayahudi na Mataifa [majina kama hayo yatatokomea].

### Ni kuhubiri kwa Masihi

Wahahudi wale wameendelea kuwa na imani katika mafundisho ya Agano la Kale wangali wanamtarajia Masihi aje awakomboe, watatiwa wivu wakati kanisa linaanza kufahamu Yesu ni nani kama MASIHI. Wakati Mataifa kweli ***"Wanahubiri na kufundisha Yesu ndiye Kristo"*** Bila kukoma, kwa hadhara na kwa kila nyumba **(Mdo 5:42),** Wayahudi watasikia na kupokezwa. Hatakama vile Wayahudi waliamini miaka ya hapo awali ya kanisa wakati mitume wa kwanza walifundisha na kuhubiri Yesu kama Masihi, wakithibitisha yakuwa "***Yesu huyu mliyemsulibisha ndiye Bwana na Kristo'*** **(Mdo 2:36),** Kwa hivyo mara tena Wayahudi watakuja kumuamini Yesu.

Itakuwa hekima ya siri zitajulikana tena na Mitume wana ***"Hubiria Mataifa utajiri wake Kristo usiopimika"*** yakuwa ***"Ushirika wa siri"*** utajulikana **(Efe 3:3, 8-9)** kwa Wayahudi na Mataifa; wataletwa pamoja katika mwili wa Masihi.

# MASIHI, MTAWALA MKUU

## SHILOH ni mtawala aliyeahidiwa

Masihi ndiye mfalme aliyeahidiwa, hivyo ni 'Aliyepakwa', yule aliyepakwa kuketi katika Enzi ya Daudi na kutawala milele. Nakala ya kwanza yake huyu atakaye tawala ni **Mwanzo 49:10** ambapo Yakobo anatabiri juu ya mwanawe Yuda, Juu ya mambo yatakayo kuja siku za mwisho.

Aya ya kwanza ya sura hii inasema ***"Yakabo akawaita wanawe, akasema, kusanyikeni ili niwaambie yatakayowapata siku za mwisho."*** Yakobo alikuwa nabii, na alikuwa na uweza wa kutabiri yatakayojili siku za mwisho.

Alisema ***"Fimbo ya enzi haitaondoka katika Yuda, wala mfanya sheria kati ya miguu yake, hata SHILOH atakapo kuja yeye mwenye milki, mbaye mataifa watamtii"***. Fimbo ya enzi ni fimbo ya mamlaka. Ni mfano wa ufalme. Katika Biblia ya Kiganda mfano ni mukuki ya Chifu, kwa kuwa lugha haina neno la fimbo ya enzi. Katika Biblia ya Kiswahili ya Afrika ya Mashariki hawatumii jina SHILOH lakini wanatumia "Yule atakaye tawala" ambayo ndiyo maana halisi ya SHILOH.

Kwa mamia ya miaka watu wa Israeli walikuwa na unabii huu mkuu ukiwaambia habari za mtawala atakaye kuja, atakaye tawala watu wote.

## Atatoka katika kabila ya Yuda

Aliye tabiriwa atakaye shika fimbo ya uongozi alikuwa atoke katika kabila ya Yuda; lakini **yeye atatawala watu wote.** Yuda ni nani? Yeye ni mmoja wa wana wa Yakobo lakini hakuwa mzaliwa wa kwanza wa Raeli ama Leah. Lakini Yakobo anasema juu yake kwamba katika siku za mwisho jambo spesheli litatendeka kupitia Yuda.

Wakati wa unabii huu kulikuwa tu na wana kumi na wawili wa Yakobo; hapakuwa na taifa kama Yuda na Israeli walioishi. Hata hivyo unabii ulikuwa wazi: Mtawala mkuu atatoka kwa Yuda kabla aje, fimbo ama utawala utaimarishwa katika Yuda. Kwa hivyo kwa utendaji kazi katika historia Mungu alimchagua Daudi kuwa Mfalme na kumwahidi ya kwamba nyumba yake itaimarishwa na mmoja kutoka nyumba yake ataketi kwenye enzi ya Daudi milele **(2 Samueli 7)**

Nyumba ya Mfalme Sauli haikuwa imewekewa kudumu. Alikuwa wa kabila ya Beyamini na hakuwa chaguo la Mungu la kwanza. Alijinyima nafasi, na mwanawe Yonathani, mridhi wa enzi ya Sauli, alitambua ya kwamba Daudi ataridhi enzi ya Israeli.

## Mwana aliyeahidiwa wa Daudi

Katika **Mdo 2:30-31 Petro** analeta ushuhuda mara mbili kuhusu kuinuka kwa Masihi kutoka kwa nyumba ya Daudi:

- Kwanza, Petro anasema ***"Daudi akiwa nabii",*** alitabiri kufufuka kwa Masihi [Daudi alitabiri mambo mengi ya Masihi hata hivyo]
- Pili, Kwamba ***"Mungu alisema kwa kiapo"*** ya kuwa Masihi atakuja kutoka kwa mbari yake.

Ahadi ya Daudi inapatikana katika **2 Samueli 7**. Mazingira ni kwamba Daudi alikuwa amejinjengea Nyumba na kisha alitaka kumjengea Mungu ambaye uwepo wake ulikuwa katika Hema ya Daudi. Mungu alinena na Daudi kupitia Nathanieli nabii na kumwaambia Daudi

kwamba ***"Atanjenga nyumba"*** yake **(aya 11).** Hii sio nyumba ya kawaida ya kukaa lakini inazungumzia mbari/ ukoo utakao kumbukwa milele. Mungu aliahidi ya kuwa mbegu ya Daudi itakuwa Masihi au yule atakaye tawala.

Mbegu ina maana gani? Inamaanisha uzao wa Daudi mmoja, mmoja kutoka kwa **nyumba** yake. Katika asiri, Sulemani alichukua enzi na kuijenga nyumba ya Mungu [Hekalu] lakini ahadi sio mwana katika asiri. Zaidi ya hayo wakati utawala wa Sulemani uliisha, Ufalme wa Daudi uligawanyika mara mbili: Israeli na Yuda. Kutoka wakati huo wa Yuda mpaka wakati ambapo yule mmoja, aliyetabiriwa kwanza kama Shiloh, atakapo kuja kutoka Yuda.

Mungu aliahidi Daudi ***"Nitainua mzao wako nyuma yako, atakayetoka viunoni mwako, nami nitaufanya imara ufalme wake, Yeye ndiye atakayejenga nyumba kwa jina langu, nacho kiti cha enzi cha ufalme wake nitakifanya imara milele. Mimi nitakuwa Baba yake, naye atakuwa Mwanangu"*** **2 Sam 7:12-14a.**

- Ahadi ni kwa mbegu ya Daudi; mbegu itaridhi ufalme.
- Ahadi hii inaongea habari za ufalme na enzi ya "**kudumu;"**
- Ahadi hii inaongea juu ya Mwana wa ahadi akiijenga **"nyumba kwa jina langu";**
- Ahadi inazungumza juu ya Mwana akiwa Mwana wa **"Baba!"**
- Mungu alithibitisha ahadi ***"Na nyumba yako, na ufalme wako, vitathibitishwa milele mbele yako. Nacho kiti chako kitafanywa imara milele"*** **2 Samueli 7:16**

## Maagano ya Mungu kwa Daudi

Ahadi alizopewa Daudi katika **2 Samueli 7** zimerudiwa katika **1 Nya 17** kuanzia **aya 10-14.** Wakati kifungo cha maandiko ama sehemu inarejelewa katika Biblia kuna ushahidi mara mbili. Niyamuhimu sana kwetu sisi kutambua ushahidi mara mbili. Petro anaonyesha ahadi hii katika **Mdo 2:30*, "Mungu amemuapia kwa kiapo [Daudi]"*.**

## Ahadi ingetimizwa namna gani?

Kama miaka 500 baada ya Daudi, ufalme wa Yuda walienda katika utumwa katika Babiloni. Mfalme wa mwisho kutawala Yuda, ambaye alikuwa ni mzao wa Daudi, alikufa katika utumwa. Wakati Wayahudi walirudi kutoka utumwa miaka 70 baadaye, hawakupata mfalme tena.

Katika siku za Yesu palikuwa na mfalme palistine, katika mji wa Yuda. Jina kake alikuwa ni Herode, na hakuwa mzao wa Daudi. Hakuwa Muyahudi halisi, alikuwa mtu aliyechanganyika. Aliingia katika enzi kwa ujaja na ujeuli; alikuwa mtu muovu, lakini alifaulu kupata kibali na Warumi, akitafuta kupata kibali na Wayahudi.

Ahadi ya Daudi iliongea njuu ya 'mwana mkuu'wa Daudi; atakaye ichukuwa enzi ya Daudi na kutawala milele. Huyu ni Masihi. Ni mfalme aliyeahidiwa. Ahadi ilikuwa ipi? Atawakomboa watu wa Mungu kutoka kwa adui wao wote.

## Ahadi imetimizwa

Wakati Petro alikuwa akihubiri siku ya pentekote, alisema, ***"Basi kwa kuwa ni nabii (Daudi) akijuwa ya kuwa Mungu amemuapia kwa kiapo, yakuwa katika uzao wa viuno vyake atamketisha mmoja katika kiti chake cha enzi"*** **(Mdo 2:30).** Petro anaonyesha kutimizwa kwa yale Mungu alikuwa ameahidia Daudi kwamba mmoja wa ukoo wake atakuwa Masihi na huyo ni Yesu ambaye walikuwa wamemsulibisha.

## Unabii wa Daudi kuhusu Masihi

Tumetazama ahadi kwa Daudi na sasa tunatakiwa kutazama neno la unabii la Daudi kumhusu Masihi. Daudi alitabiri mambo kumhusu Masihi, na Mungu aliahidi Daudi mambo kumhusu Masihi.

## Kuhusu Masihi katika Zaburi 110

Yesu aliwauliza Mafarisayo ***"Mwaonaje katika habari za Kristo? Ni mwana wa nani? Wakamwaambia ni mwana wa Daudi; Imekuwaje basi Daudi katika Roho kumwita Bwana akisema, BWANA alimwambia Bwana wangu, Uketi mkono wangu wa kuume, Hata niwawekapo adui zako kuwa chini ya miguu yako? Basi Daudi akimwita Bwana imekuwaje?"*** **Mathayo 22:41-45.** Yesu alikuwa akinukuu kutoka kwa **Zaburi 110** ambayo ni mojawapo wa Zaburi za wazi za Masihi katika Zaburi, hivyo ni Zaburi zinazozungumza juu ya kuja kwake Masihi na katika hali ya **Zaburi 110,** utawala wake wa uungu.

Kisha Daudi anasema ***"BWANA atainyosha toka Sayuni Fimbo ya nguvu zako. Uwe na enzi kati ya adui zako"*** **aya 2.** Masihi aliyetarajiwa atatawala katika Sayuni, hata kati ya adui zake.

Kisha katika **aya 3**, maandiko yanasema, ***"Watu wako wanajitoa kwa hiari, siku ya uweza wako."*** Hii inafanya kazi siku zetu. Watu wengi wa Mungu wajihisi kana kwamba wanatawaliwa na hari zao za kikanisa. Yesu anawaita watu kwa hiari na katika miungano ya kiutume ambayo inainuka, sisi tu watu ambao wanajitoa kwa hiari, tukijifurahisha katika kumtumikia Masihi na kutembea katika utiifu katika kumtii yeye

Katika **Zaburi 110:4,** Daudi pia anadhihirisha yakwamba huyu mfalme mtawala atakuwa hakika ***"Kuhani hata milele kwa mfano wa Melkizedeki"***. Haya yamedhibitishwa katika **Zakaraya 6: 11-13,** ambapo kuhani mkuu Joshua amevikwa taji na kuketishwa kwenye enzi, akitawala, ***"Yeye ndiye atakaye ijenga Hekalu ya YAHWEH"***. Hakika Yesu ameyatimiza haya na unabii wote wa Masihi

Mwandisi wa Zaburi anaongea juu ya mamlaka na hukumu ambayo imepatianwa na Masihi, ambayo itaadhiri wafalme na Mataifa na nchi nyingi (**5-6).** Katika hukumu hii ***"Atakunywa maji ya mto njiani; kwa hiyo atakiinua kichwa chake"*** **aya 7**

## Mfame ambaye Mungu ataweka Sayuni

Katika **Zaburi 2.** Daudi anatabiri juu ya mfalme atakayekuja, Mataifa wako katika uasi kinyume cha Mungu ***"Kinyume chake yeye aliyepakwa"*** (**aya 1-3**). Jawabu ya Mungu ni kwamba kwanza anacheka, kisha anakaa kama hajamaanisha, kisha ghadhabu **(aya 4-5**). Na kisha Mungu anainukia mataifa walioasi na wafalme wao, ***"nimemweka mfalme wangu juu ya Sayuni, mlima wangu mtakatifu"*** (**aya 6**). Ahadi ya Masihi, ahadi ya mtawala mkuu, [SHILOH] Sasa unachukuwa mwelekeo. Mungu atainua mfalme huyu na kuuweka ufalme uwe juu yake milele.

Kisha katika **aya 7,** Sio YAHWEH, anaongea lakini Masihi, Mwana, anenapo anasema ***"Nitaihubiri amri; BWANA, aliniambia, ndiwe mwanangu, leo nimekuzaa".*** Mungu alimuambia Daudi kupitia nabii, Yakuwa YAHWEH atapata mtoto Mwana ambaye atakuwa mfalme. Yeye ndiye mfalme atakayewekwa kwenye enzi, hakika yeye ni Mwana wa Mungu. Mwana ana uridhi hapa ulimwenguni, ***"Uniombe, nami nitakupa mataifa kuwa urithi wako, na miisho ya dunia kuwa milki yako"*** (**aya 8**). Yeye ana mamlaka ***"ya kuwaponda kwa fimbo ya chuma, na kuwavunja kama chuma cha mfinyanzi"*** (**aya 9**). Kisha **aya 10-12** anawaonya

wafalme na waamuzi ***"wamtumikie BWANA kwa kicho"*** na ***"kushika yalio bora, asije akafanye hasira nanyi mkapotea njia"***.

### MASIHI NI NANI?

- Yeye ndiye mfalme
- Mungu atamuweka kwenye enzi
- Hakika yeye ndiye mwana wa Mungu
- Yeye ana urithi hapa duniani: Mataifa
- Ana mamlaka kamili ya kuadibu Mataifa
- Wafalme wote na waamuzi watamtumikia

### Na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake

***"Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, Tumepata mtoto mwanamume; Naye ataitwa jina lake, Mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani. Maongeo ya enzi yake na amani hayatakuwa na mwisho kamwe, katika kiti cha Daudi na ufalme wake; kuuthibitisha na kuutegemeza kwa hukumu na kwa haki, Tangu sasa na hata milele, wivu wa Bwana wa majeshi ndio utakaotenda hayo"*** **Isaya 9:6-7**.

Isaya anatabiri juu ya kuja kwa Masihi. Alizaliwa kama mtoto lakini amepatianwa kama Mwana na uweza wa kifalme utakuwa Wake. Jina Serekali halionekani mara nyingi katika maandiko. Jina linaloonekana mara nyingi linaonyesha uweza wa kifalme ni jina 'ufalme'. Nihaki kufahamu 'Serekali' katika aya hii inatoshana na Ufalme wa Mungu lakini kifungu kinataka tufahamu yakuwa serekali ya Masihi ni ya Kweli kabisa na ya wakati huo. Yesu ndiye ***"Mkuu wa wafalme wa dunia"*** **Ufu 1:5**.

Serekali ya Masihi inaendelea kuongezeka. Wengi wanangojea 'utawala wa Karne' wa Kristo lakini hawaelewi yakuwa ***"Amepandishwa hata mkono wa kuume wa Mungu"*** (**Mdo 2:33**) alipopaa juu.

### Yesu ameketi katika enzi

Yesu alikuja kama Masihi kutayarisha kuthibitishwa kwa ufalme wa Mungu hapa duniani. Kazi yake ilikamilika wakati alipoketi katika mkono wa kuume wa Baba, baada ya kufufuka kutoka kwa wafu (**Efe 1:20).** Mkono wa kuume wa Mungu inaongea juu ya mamlaka ya pahali hapo, hivyo ni, nafasi. Yesu ameketi kwa enzi, sio kiti cha chini kwa mkono wa kuume wa Baba, Kuna enzi moja tu mbinguni na ndio Mungu ameketi katika enzi hio, lakini ni Yesu mtu aketiye katika enzi hio: ***"Maana sharti amiliki yeye, hata awaweke maadui wake wote chini ya miguu yake"*** **1 Kor 15:25.** Kama Masihi, Yesu ana mamlaka yote mbinguni na duniani (**Mat 28:18**).

# YESU WA NAZARETI NDIYE KRISTO

## KUMTANGULIZA YESU

### Utabiri wa Malaika gabrieli

***"Tazama, utachukuwa mimba na kuzaa mtoto mwanamume; na Jina lake utamuita Yesu. Huyu ataitwa mkuu, ataitwa mwana wa aliye juu, na Bwana Mungu atampa kiti cha enzi cha Daudi, baba yake. Ataimiliki nyumba ya Yakobo hata milele, na ufalme wake hauna mwisho"* Luka 1:31-33**.

### Malaika alitangaza

Malaika wa Mungu aliyesimama mbele ya wachungaji juu ya uwanja, alisema "***Msiogope; kwa kuwa mimi nimewaletea habari njema ya furaha kuu itakayokuwa kwa watu wote; maana leo katika mji wa Daudi, amezaliwa, kwa ajili yenu, Mwokozi, ndiye Kristo Bwana"* (Luka 2:8-11)**.

### Simeoni alimtambua Masihi

***"Na tazama, pale Yerusalemu palikuwa na mtu, jina lake Simeoni, naye ni mtu mwenye haki, mcha Mungu, akitarajia faraja ya Israeli; na Roho Mtakatifu alikuwa juu yake, Naye alikuwa ameonywa na Roho Mtakatifu ya kwamba hataona mauti kabla ya kuona Kristo (Masihi) wa Bwana*" Luka 2:25-26.** Simeoni alimtambua mtotoYesu kama Masihi, na vile vile Anna yule nabii mke **(Luka 2:36-38).**

### Wale mamajuzi walianguka chini na kumuabudu yule mtoto

***"Yesu alipozaliwa katika Bethlehemu ya Uyahudi zamani za Mfalme Herode, tazama mamajuzi wa mashariki walifika Yerusalemu, wakisema, yuko wapi aliyezaliwa mfalme wa Wayahudi? Kwa maana tuliiona nyota yake mashariki, nasi tumekuja kumsujudia.***

***Wakaingia nyumbani wakamsujudia; nao walipokwisha kufungua hazina zao, wakamtolea tunu; dhahabu na uvumba na manene"* Mat 2:1-3, 11.**

## UFUNUO WA YESU WA NAZARETI KAMA MASIHI

### Matendo sura ya pili

Wahubiri wengi wa kipentekote na wa karismatiki wanatumia **Mdo 2** kuwafunza watu juu ya ubatizo wa Roho Mtakatifu na kupokea karama za lugha. Bali kwa uhakika **mdo 2** kimsingi ni mahubiri yenye nguvu ya kuoyesha kutoka maandiko ya Agano la kale, ya kudhibitisha Yesu wa Nazareti ni Masihi aliyeahidiwa.

### Siku ya pentekote

***"Hata ilipofika siku ya Pentekote"* (Mdo 2:1),** Roho Mtakatifu alikuja kutimiza siku kuu, ambayo wayahudi walikuwa wakisherehekea toka wakati Mungu alimtokea Musa katika mlima wa Sinai na akampatia sheria. Sasa ilikuwa ni siku ya sherehe kutimizwa. Sasa angetimiza siku ya pasaka kwa kufa msarabani akifufuka kutoka kwa wafu. Sasa angetimiza sikukuu ya pasaka kama vile alivyo waahidi wanafunzi kwa kutuma Roho Mtakatifu.

Roho Mtakatifu alikuja kwa ishara na maajabu:

- ***"Kukaja ghafla toka mbinguni uvumi kama wa upepo wa nguvu ukienda kasi"***
- ***"Kukatokea ndimi zilizo gawanyika za moto"***
- ***"Wote wakajazwa Roho Mtakatifu na wakaanza kunena kwa lugha"***

Kana matokeo ya kujazwa kwa Roho, wanafunzi waliotoka Galilaya walikuwa na uweza wa kuongea lugha ambayo hawakujifunza. Kulikuwa na Wayahudi waliojitoa katika Yerusalemu kwa sikukuu kutoka miji kumi na sita tofauti na ***"Kwa kuwa kila mmoja aliwasikia wakisema kwa lugha yake mwenyewe ... Matendo makuu ya Mungu"*** **(Mdo 2:6-11).**

Petro alieleza juu ya kumwagwa kwa Roho Mtakatifu ambayo ilitokea siku hio ya ajabu kwa kunukuu **Yoeli** Katika **Mdo 2:16-21.** Kisha anaonyesha kwamba Yesu amepanda juu ya enzi ***"na kupokea kwa Baba ile ahadi ya Roho Mtakatifu*** **(aya 33)**

## Mambo muhimu juu ya Yesu

Petro anapatiana habari juu ya maisha ya Yesu kwa mktasari

- **Mtu huyo na huduma yake**

***"Enyi waume wa Israeli, sikilizeni maneno haya; Yesu wa Nazareti, mtu aliyedhihirishwa kwenu kwa Mungu kwa miujiza na ajabu na ishara, ambazo Mungu alizifanya kwa mkono wake kati yenu, kama nyinyi wenyewe mnavyojua"*** **Mdo 2:22.** Jambo la muhimu sana analo linena juu ya Yesu ni kwamba Yesu alikuwa Mtu wa Mungu; alikuwa mtenda miujiza; yakuwa ishara na maajabu zilitendeka na zilikuwa ni dhibitisho kwamba Mungu alikuwa naye. Mambo makubwa yalitendeka: watu walifufuka kutoka kwa wafu; watu wenye magonjwa mabaya kwa muda mrefu waliponywa; watu walikombolewa kutokana na pepo wasubufu; watu maelfu walilishwa; katika kalamu ya harusi aligeuza maji kuwa divai. Alikuwa na sifa; alishuhudiwa kuwa ni Mwana wa Mungu.

- **Kifo chake**

***"Mtu huyu alipotolewa kwa shauri la Mungu lililokusudiwa, na kwa kujua kwake, ninyi mkamsulibisha kwa mikono ya watu wabaya wakamwua"*** **aya 23.** Jambo lingine muhimu ni kwamba watu wabaya walimchukua Yesu wakamsulibisha, wakamuua. Alikufa, na kifo chake kilikua cha jambazi, hakika alisulibishwa: Hicho ndicho ambacho kilikuwa cha kushtua sana na ambacho hakikukubalika kabisa ambacho Warumi walikua wakiuana. Lakini kifo chake kilikua ni kwa kadiri ya kusudi la Mungu alilolijua kwanza.

- **Kufufuka kwake**

**"*Ambaye Mungu alimfufua, akiufungua uchungu wa mauti, kwa sababu haikuwezekana ashikwe nao"*** **Mdo 2:24.** Mungu alimuinua Yesu! Alifufuka!

Kuna mambo matatu muhimu:

**i.** Hakika Yesu alikuwa Mwana wa Mungu; alikuwa mtenda miujiza, ishara na miujiza zilifanyika kwake siku za maisha yake
**ii.** Alichukuliwa na watu wabaya wakamsulibisha, kulingana na mapenzi ya Mungu
**iii.** Mungu alimfufua kutoka kwa wafu.

## KUFUFUKA KWA YESU

### Daudi alitabiri ufufuo

Petro katika **Mdo 2:25-28** Alinukuu Daudi katika **Zaburi 16,** ***"Kwa maana Daudi anasema kumhusu".*** Anatumia maandiko ya Agano la kale na kutumia ufahamu uliojulikana yale yaliokuwa yametendeka Yerusalemu hivi karibuni. ***"Nalimwona YAHWEH mbele yangu sikuzote, kwa kuwa yuko upande wa mkono wangu wa kuume, nisitikisike. Kwa hiyo moyo wangu ukapendezewa, ulimi wangu ukafurahi; Tena mwili wangu ukakaa katika matumaini. Kwa maana hataiacha roho yangu katika kusimu wala hutamtoa mtakatifu wako aone uharibifu."***

Kusimu ndio jina la pahali pa wafu; katika agano jipya inaitwa Sheol. Hii ni Zaburi ya kiunabii ikionyesha kufufuka kwa Mtakatifu wa Mungu. Nafsi inaishi kusimu, lakini mwili unapata uharibifu katika kaburi. Daudi anasema kwamba kuna mmoja ambaye nafsi yake haitakaa kusimu; wala mwili wake kuwachwa kaburini kuona uharibifu. ***"Umenijulisha njia ya uzima, utanijaza furaha kwa uso wako"*** **aya 28.**

***"Waume, ndugu zangu mniwie radhi, niseme kwa ujasiri mbele yenu habari za baba yangu mkuu, Daudi, yakuwa alifariki akazikwa, na kaburi lake liko kwetu hata leo"*** **aya 29.** Wayahudi wote walijua kuwa Daudi alikufa kifo cha kawaida mamia ya miaka iliyokuwa imepita na kaburi lake lilikuwa lingali Yerusalemu.

### Ni kufufuka kwa Kristo

**"*Basi kwa kuwa yeye ni nabii, -*** Daudi alikuwa na uweza wa kueleza yatakayojiri ***"Akijua yakuwa Mungu amemuapia kwa kiapo, yakuwa katika uzao wa viuno vyake atamketisha mmoja katika kiti cha enzi"*** **(aya 30).** Tumeshuhudia ushahidi mara mbili wa neno la kiunabii na kiapo kutoka kwa Mungu. Daudi alijua kutoka kwa Mungu, na kisha alijua kutoka kwa unabii ya kwamba Masihi atatoka kwake ***"Kulingana na mwili"***.

Daudi pia alitabiri vyema kufufuka Katika **Zaburi 16,** na Petro pia alitabua kwamba alikua akitabiri kufufuka kwaYesu na huyu ni Yesu wa Nazareti. ***"Yeye,*** [Daudi] ***akitangulia kuyaona haya, alitaja habari ya kufufuka kwake Kristo, yakwamba roho yake haikuachwa kuzimu, wala mwili wake haukuona uharibifu.*** **(Aya 31)** Kulingana na Petro, unabii wa Daudi katika zaburi umetimizwa kwa sababu alitazamia wakati wa Masihi na Petro anasema ya kwamba Mungu hakuacha nafsi ya Masihi kuzimu; Mungu hakukubali mwili wa masihi uharibike.

### Yesu alifufuka kutoka kwa wafu

**"*Yesu huyu Mungu alimfufua, na sisi tu mashahindi wake"* Aya 32.** Petro alikuwa amemtambulisha Yesu katika **aya 22-24,** Kisha akatoa andiko la kinabii kudhihirisha yakuwa Masihi angekuwa mzao wa Daudi na angefufuka kutoka kwa wafu. Sasa anatangaza yeye na wanafunzi wengine wa Yesu walikuwa mashahidi wa kufufuka kwa Yesu, wakidhihirisha kuwa Yesu ndiye Masihi.

### Kuja kwa Roho Mtakatifu ni thibitisho

***"Basi yeye [Yesu] akiisha kupandishwa hata mkono wa kuume wa Mungu, na kupokea kwa Baba ile ahadi ya Roho Mtakatifu, amekimwaga kitu hiki mnachokiona na kusikia"*** **Aya 33.** Mkono wa kuume wa ***Mungu*** unaonyesha enzi ya Mungu. Mkono wa kuume wa Mungu ni mahali pa nguvu na mamlaka. Petro anatangaza ya kwamba kumwagwa kwa Roho Mtakatifu

kungekuja baada ya Masihi kupandishwa kwenye enzi. Kuthihirishwa kwa Roho Mtakatifu ni thibitisho ya kuwa Yesu ni Masihi na amepandishwa kwenye enzi.

***"Maana Daudi hakupanda mbinguni; bali yeye mwenyewe anasema, Bwana alimwambia Bwana wangu, keti mkono wangu wa kuume. Hata nitakapowaweka adui zako chini ya miguu yako"*** **Mdo 2:34-35.** Petro ananukuu **Zaburi 110** na akionyesha wazi kuwa Masihi ametimiza unabii. Amepandishwa kwenye enzi; Ameketi pahali pa mamlaka; na sasa maadui wake wote watakabilianwa nao.

## Yesu ndiye Bwana na Kristo

Agano la kale linatufundisha YAHWEH ndiye Bwana [Adonai]. Adonai ndiye kichwa kinachotumika kikimuonyesha Bwana wa utukufu katika uweza na nguvu. Wayahudi walitumia kichwa hiki wakitaja jina la Bwana kwa maana hawakutumia jina la Mungu. Inatoka kwa neno *adon* ambayo inamaanisha 'mwenyewe, Bwana mkuu; inaonyesha bwana wa watu na Bwana wa kiungu'. {Strongs Concordance # Heb 113} Katika Agano jipya neno la kiyunani la Bwana ni *Kurios* {SC# Gr.2962} inamaanisha 'mwenyewe, bwana, mwelekezi, aliye na mamlaka'. Baadhi ya wafafanuzi wanapendekeza kuwa Kurios ni kichwa cha kiyunani kikionyesha YAHWEH [YHWH] imetafsiriwa kama BWANA. Katika tafsiri ya Agano ya kale ya kiyunani (Septuagint) kabla ya Kristo, hili neno Kurios lilitumika kama kichwa cha Jina la Mungu.

Petro alipotangaza: ***"Basi nyumba yote ya Israeli nayajue yakini ya kwamba Mungu amemfanya Yesu huyo mliye msulibisha kuwa Bwana na Kristo"*** **Aya 36.** Alikuwa akipatiana uungu wote kwa Yesu. Ambacho Petro amethibitisha ni kwamba Masihi aliyeahidiwa wa Agano la kale ni Yesu wa Nazareti. Ametangazwa na Mungu kuwa "***Bwana na Kristo"***. Petro hamtangazi Yesu kuwa Kristo, Masihi aliyetarajiwa kuja tu, walakini anamtangaza Yesu kuwa Bwana wa yote. Petro alikuwa akipatiana uongozi wote wa Mungu kama Yahweh katika Agano la kale kwa Yesu katika Agano jipya. Ulikuwa ni ujumbe ulioleta ushawishi na mabadiriko ya wayahudi 3000 siku hiyo.

Petro mtume alikuwa katika ufahamu wa unabii mwingi wa Agano la kale, na kizazi chake chote kikamhisi Masihi. Masihi alitarajiwa kuja wakati huo. Twajua kutoka **Yohana 1** ya kwamba nduguye petro Anderea, baada ya kumuona Yesu, moja kwa moja aliend akampata petro, na akamwambia ***"Tumempata Masihi",*** Yeye ni Yesu wa nazareti. Filipo akafanya vivyo hivyo: akaenda akamwambia Nathanieli.

## Kanisa linajengwa katika ufunuo

Kanisa linajengwa katika ufunuo wa kumjua Yesu. Kanisa linajengwa katika ufunuo wa Yesu kuwa Masihi na Mwana wa Mungu. Hivyo ndivyo petro alisema, ***"Wewe ndiwe Kristo [Masihi] Mwana wa Mungu aishiye"*** **Mathayo 16:16.** Ni katika msingi huu wa ufunuo wa petro ambapo Yesu alisema ***Na ninakwambia, wewe ndiwe petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu, wala milango ya kuzimu haitalishinda"*** **aya 18.** Kujengwa kwa kanisa na Yesu inategemea ufahamu wa unabii wa Yesu katika Agano la kale. Yesu alikuwa na uwezo wa kutangaza ya kwamba ataanza kulijenga kanisa.

## Bwana ni nani?

Swala la Bwana wa kanisa lilikuwa la umuhimu mkubwa sana kwa karne tatu zilizo fuata. Serekali ya Kirumi ilitangaza na ikahimiza kwamba Rumi yote ilikuwa imtambue Kaisaria kama Bwana! Wakristo walikataa kwa maana walikuwa na ufunuo wenye msukumo na

ushawishi kwamba Bwana pekee mbinguni na duniani ni Yesu. Kwa ushawishi huu wakristo wengi walifanyika wafia dini. Walipatwa na hatia na mawakiri Wakirumi na wakahukumiwa kifo kwa njia iliyo baya na ya kuogofya sana.

### Mwili wa Kristo

Yesu alisema atalijenga kanisa lake na maandiko yafunua ya kwamba kanisa ni mwili wa Kristo. Twastahili kufahamu ya kwamba kanisa kabisa ni mwili wa Masihi, mfalme anayetawala. Kiyahudi katika Agano jipya chaita kanisa 'kundi la masihi'. Neno la kiyunani *ekklesia* lamaanisha wale *walioitwa.* Kanisa lasungumzia watu ambao ni wa Yesu aliye Masihi.

Maandiko yasema wazi, ***"naye ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha kanisa;*** **(Wakolosai 1:18).** Kanisa ni ***"Mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote*** **(Waefeso 1:23).** Kristo kwa kupaa kwake "***juu sana kuliko ufalme wote na mamlaka, na nguvu, na ushultani"*** **(Aya 21)** alipatianwa awe ***"Kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa"*** **(Aya 22).**

Paulo anaendelea katika **1 Wakorintho** akituambia kanisa imejengwa ***"na viungo vya mwili mmoja, navyo ni vingi"*** **(12:12),** kwa hivyo Kristo ni **viungo vingi vya mwili!** Kama kanisa ni mwili wa masihi, kama kanisa hakika limeunganishwa kwa Masihi kama mwili kwa kichwa chake, basi huo mwili unakuwa mwili wa watu waliounganishwa kwa mfalme anayetawala.

***"Kristo ndani yenu tumaini la utukufu"*** **Wakolosai 1:27.** Ufunuo wa siri ya utukufu wa Mungu ni ufunuo wa Kristo katika mwili, kanisa. **'Mfalme anaishi katika ngome ya moyo wangu'.** Hivyo ndivyo tulivyoimba katika siku za kiroho lakini hatukufahamu undani na nguvu za ukweli huo! Mfalme wa wafalme anaishi ndani ya moyo wangu. Yuko ndani yangu na mimi niko ndani yake! Ni kupitia mwili wa Kristo ambapo utukufu wa Mungu utafunuliwa ulimwenguni na kila nafsi itajua kwamba Yesu aliye Masihi ndiye Bwana kwa utukufu wa Mungu.

# MWANA WA MUNGU

***"Mwanzo wa injili ya Kristo, Mwana wa Mungu"*** **Mariko 1:1**

Tumetazama kwa kifupi **mwanz**o wa **injili** na injili ni nini; tumetafuta kuelewa kiundani na maana ya nguvu ya jina **Yesu,** na kuthibitisha yakuwa alikuwa mwana wa adamu; na tumechunguza kwa makini unabii wa Masihi na ahadi za agano la kale ambazo zilitimizwa ndani ya Yesu na ambazo zinathibitisha Umasihi wake, yakuwa Yesu ni **Kristo.** Katika sura hii tunataka kuelewa 'jinsi Yesu alivyo Mwana wa Mungu'; na inamaanisa nini kusema **'Yesu ni Mwana wa Mungu'**.

## Mwana wa Mungu wa kwanza katika historia

**"*Hiki ndicho kitabu cha vizazi vya Adamu. Siku hile Mungu alimuumba mtu, kwa sura ya Mungu alimfanya"*** **Mwanzo 5:1** Adamu akimaanisha binadamu, aliumbwa kwa mfano wa Mungu, ***"Mwanamume na mwanamke aliwaumba"*** **(Mwanzo 1:27)**. Adamu anaitwa ***"Mwana wa Mungu"*** **(Luka 3:38).** Adamu ni mwana wa Mungu; Mungu ni Baba wa Adamu; adamu hakuzaliwa aliumbwa. Hii ni ya maana kuifahamu:

**Adamu ni Mwana wa Mungu sio kwa kuzaliwa kiasili, lakini ni kwa maumbile na mpangilio wa maumbile.** Tunaweza kusema Adamu na Hawa 'waliwekwa kuwa wana na Mungu. Hawakuzaliwa kama watoto lakini waliumbwa katika ukomavu katika utu wao unaoonekana.

Adamu kama mwana wa kwanza aliumbwa kwa sura na mfano wa Mungu. Yesu kama adamu wa mwisho alikuwa ***"Mungu alidhihirishwa katika Mwili"*** **1 Timotheo 3:16.** Mungu alipo dhihiriswa katika mwili Yesu alikuwa hana dhambi na katika ukomavu wake kama mwana alidhihirisha kikamilifu sura na mfano wa Mungu kwa mwanadamu.

## Vizazi vya Yesu

Vizazi vyaYesu katika **Luka 3** inamuunganisha Yesu katika mwili akiwa katika mbali ya Adamu ambaye alikuwa ***"Mwana wa Mungu".*** Hata katika mbali ya kiasiri Yesu alikuwa wa uzao wa adamu ambaye alikuwa mwana wa Mungu.

Katika vizazi ndani ya **Mathayo** Yesu ako katika mbali ya Daudi na Abrahamu haswa. Hii ni ***mbali ya kiroho kinyume na ile mbali ya kiasili katika Luka. Daudi kama mfalme aliyechaguliwa*** ana sehemu maalum katika ufalme wa Mungu na Yesu **'ndiye Mwana wa Daudi aliye tabiriwa'.** Katika kuunganisha Yesu na Abrahamu, Mathayo anaonyesha mahali pake spesheli kama **'mbegu iliyoahidiwa'.** Mungu alikuwa ameahidi kupitia mbegu /mwana wa Abrahamu ***"jamaa zote za dunia watabarikiwa"*** **Mwanzo 12:3**

**Mathayo 1:1** Inamtambua Yesu kama Masihi, Mwana wa Daudi na Mwana wa Abrhamu. Katika **Mdo 2:30**, Petro anapatiana ushahidi kuwa Yesu ni Mwana wa Daudi. **Warumi 1:2-3** Yaongea juu ya Mwana aliyeahidiwa hapo awali ***"Kwa kinywa cha manabii wake katika maandiko matakatifu"*** na kudhibitisha kuwa Yesu ni Mwana wa Daudi "***aliyezaliwa katika ukoo wa Daudi kwa jinsi ya mwili."*** **Aya 4** inathihirisha kwa ***"uweza kuwa Mwana wa Mungu, kwa jinsi ya roho ya utakatifu, kwa ufufuo wa wafu".***

## Mwana wa Ibrahimu

Ibrahimu alikuwa na wana wawili katika asiri: Mmoja wa mwanamke mtumwa, Ishmaeli, na mwengine mwana wa ahadi, Isaka, lakini alizaliwa kiasiri. Mbegu ya ahadi ama mwana

aliyeahidiwa atakaye ondoa laana ambayo Adamu alileta kwa watu wote angekuja. Mwana wa tatu wa Ibrahimu hakika ni **mbegu** na hiyo ni Kristo ambaye ni Yesu. **Wagalatia 3:16** Inatuambia ahadi zilifanywa ***"kwa Ibrahimu na kwa mzao wake. Hasemi, kwa wazao kana kwamba ni wengi bali kana kwamba ni mmoja, yaani Kristo."***

## Ahadi kwa Daudi

Mungu alimuahidi Daudi kwamba mmoja 'wa uzao wako' atakuwa Masihi lakini katika mazingira ya kufanya ahadi hiyo kwa Daudi, Mungu akasema ***"mimi nitakuwa baba yake, naye atakuwa mwanangu"*** **2 Samueli 7:14.** Mbegu ya Daudi [Uzao] atakuwa mwana wa Mungu **(1 Nya 17:13a).** Kitabu cha **Waebrania 1:5b** cha nukuu aya hii katika **Samueli,** ikiweka wazi yakuwa Mwana wa Mungu ndiye anayetajwa katika ahadi ya Daudi.

## Unabii wa Daudi

Katika **Zaburi 2** Daudi alitabiri mfalme ambaye Mungu ataweka Sayuni atakuwa ni Mwana wa Mungu: ***"Nitaihubiri amri; BWANA (Yahweh) aliniambia, ndiwe mwanangu, mimi leo nimekuzaa"*** **aya 7**. Tena katika kitabu cha **Waebrania 1:5a** ni wazi: inaongea juu ya Mwana wa Mungu ambaye ni Yesu.

Yesu hangefanyika mwana wa Mungu kwa kuzaliwa kwa jia ya kiasiri ijapokuwa ***"Azaliwa na kuwa mbegu ya Daudi kwa jia ya mwili."*** Daudi anasema katika zaburi kwamba Mwana **'alizaliwa,'!** Paulo anasema katika **Filemoni 10** yakuwa Onesimo ni ***"mtoto wangu niliyemzaa katika vifungo vyangu."***

Uwana unapatianwa kwa kuzaliwa kiroho. Mungu alitangaza wakati Yesu alipokuja kutoka maji ni alipobatizwa, ***"Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninaye pendezwa naye"*** **Mathayo 3:17.**

Wakati huo Yesu alifanyika kuwa Mwana aliyedhihirishwa: ilikuwa ni kupatikana kwa Mungu kutoka kwa Mungu na Roho.

Malaika alisema kwa Yusufu, ***"Mimba yake ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu"*** **(Mathayo 1:20).** Malaika alimwambia Mariamu, ***"Roho Mtakatifu atakuja juu yako, na nguvu zake Aliye juu zitakufunika kama kivuli; kwa sababu hiyo hicho kitakachozaliwa kitaitwa kitakatifu, Mwana wa Mungu."*** **Luka 1:35.** Yesu alizaliwa kama Mwana wa kiasiri lakini mimba yake ilikuwa ni kwa ***kupatikana kwa kiroho***

Malaika alitangaza kwa wachungaji, ***"Maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa, kwa ajiri Yenu Kristo Bwana,"*** **Luka 2:11.** Wote Semioni na Anna walimtabua mtoto Yesu aliye Masihi (**Luka 2:25-38).**

## Unabii wa Isaya

**Isaya** alitabiri yakwamba mwana spesheli atazaliwa, na huyu mtoto atapatianwa kama 'mwana' Mwana ataitwa, ***"Mshauri, Waajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani,"*** **aya 6.** Huyu Mwana ndiye Masihi ambaye atakuwa mtawala. Mwana ndiye atakayetawala walakini sio Mtoto. Nijambo la kuhuzunisha kwamba katika historia kanisani watu kwa jumla mwaka baada ya mwaka watu wanamuabudu mtoto Yesu, wakati wote wakipuuza amri ya Kristo Mwana wa Mungu.

Isaya pia alitabiri ***"Bikira atachukua mimba, atazaa mtoto mwanamume, naye ataitwa jina lake Imanueli"*** **(Isaya 7:14).** Malaika alimuelekeza Yusufu kwamba mimba ya Mariamu ilikuwa ni kutimizwa kwa unabii na **Mathayo** anasema Emanueli inatafsiriwa ***"Mungu pamoja***

***nasi”*** **(Mathayo 1:20-23).** Mwana aliyekuwa azaliwe na Mariamu angekuwa ***“Mungu aliyedhihirishwa katika mwili”*** **(1 Timotheo 3:16).**

### Unabii wa Hosea

***“Israeli alipokuwa mtoto, nilikuwa nikimpenda, nikamwita mwanangu atoke misri”*** **Hosea 11:1.** Yesu alipelekwa Misri kama mtoto kulingana na maagizo ya malaika kwa Yusufu katika ndoto, ***“Ondoka, umchukue mtoto na mama yake, ukimbilie Misri, ukae huko hata nikuambie; kwa maana Herode anataka kumtafuta mtoto amuangamize”*** **Mathayo 2:13.** ***“Akaondoka akamchukua mtoto na mama yake usiku, akaenda zake Misri akakaa huko hata alipokufa Herode, ili litimie neno lililonenwa na Bwana kwa ujumbe wa nabii, akisema, ‘kutoka misri nalimuita mwanangu”’*** **Mathayo 2:14-15.**

Mathayo anatuonyesha ya kwamba Yesu ndiye utimilifu wa maandiko ambayo yanaonyesha Mwana wa Mungu. Wakati maandiko yalitimizwa Yesu alipokua mtoto, katika tukio la kwanza Israeli walikuwa mtu walioshikana waliotolewa kutoka Misri na Mungu. Kwa hivyo ni harali kuelewa yakwamba kuonyeshwa huku kwa Yesu akitoka Misri kama mtoto ndani yake kuna ufahamu wa kiunabii wa mwana wa Mungu alieunganika ikidhihirika **(Warumi 8:19**) katika dunia (au nje ya dunia).

Je, ‘Mtoto’ na ‘Mwana’ yasungumzia mtu mmoja? Kumbuka Isaya alisema, ***“Mtoto atazaliwa, ilhali Mwana atapeanwa”*** na alikuwa akiongea kuhusu mtu mmoja. Tena Mathayo anasema kuwa mtoto Yesu anayekuja kutoka Misri hakika ni Mungu akimuita Mwanawe kutoka Misri. Wakati wote ndani ya mtoto kuna nguvu za kufanyika Mwana aliyekomaa (**Yohana 1:12**).

Mwana ni nani? Mwana ni mtoto aliyekomaa, mwana wa kiume aliyekomaa katika hali hiyo, aliyefikia umri wa kurithi; huyu ndiye anachaguliwa kama mwana. Kwa hivyo, huyu ndiye atapokea urithi; huyu ndiye atathihirishwa duniani **‘kama wana wa Mungu’.**

### Mtoto lazima akomae

Jambo kubwa la kuelewa katika uwana ni kwamba Mwana ni mtoto kijana aliyekomaa. ***“Mrithi, wakati wote awapo mtoto, hana tofauti na mtumwa, angawa ni bwana wa yote…hata wakati uliokwisha kuamriwa na baba”*** **Wagalatia 4:1-2.** Hii ilionyesha wazi katika maisha ya Bwana Yesu: wakati alipokuwa mtoto watu wachache sana walimtambua. Hata kama kijana watu wachache sana walimjua; lakini katika umri wa miaka 30 alithihirishwa kama Mwana.

### Yesu kama Mwana

Katika ukomavu wake, ambao ulianza katika ubatizo wake, Yesu alitembea na Baba yake katika njia ya ajabu sana. Alisema ***“Baba yangu anatenda kazi hata sasa, nami ninatenda kazi. Mwana hawezi kutenda neno mwenyewe ila lile ambalo amuona Baba analitenda; kwa maana yote ayatendayo yeye, ndiyo ayatendayo Mwana vile vile. Kwa kuwa Baba ampenda Mwana naye humuonyesha yote atendayo mwenyewe; hata na kazi kubwa zaidi kuliko hizo atamuonyesha, ili nyinyi muweze kustaajabu”*** **Yohana 5:17, 19-20.**

***“Ili watu wote wamheshimu Mwana kama vile wanamheshimu Baba. Asiyemheshimu Mwana hamheshimu Baba aliyempeleka”*** **Yohana 5:23.**

Katika **Yohana 14,** Yesu anaongea wazi kwa wanafunzi wake ijapokuwa walikuwa na shinda ya kuelewa vile alisema, ***“Aliyeniona mimi amemuona Baba; basi wewe wasema aje utuonyeshe Baba? Husadiki kwamba mimi ni ndani ya Baba, na Baba yu ndani yangu?”*** **Aya 9-10.**

Yesu aliendelea kuongea habari ya Baba yake na akamtaja Mungu kuwa Baba zaidi ya mara 170 katika injili. Yesu alisema Mungu ni Baba yake. Yesu alimjua Mungu kama Baba yake, haswa kutoka wakati wa ubatizo wake alipopokea ***"Roho wa Mwanawe"*** **(Wagalatia 4:6).** Wakati mbingu zilimfungukia Yesu wakati wa ubatizo wake, alipokea Roho wa Baba yake bila kipimo (**Yohana 3:34).**

Yule akida aliyehusika katika kuawa kwa Yesu, baada ya ulimwengu kutetemeka, alisema, ***"Hakika huyu alikuwa ni Mwana wa Mungu!"*** **Mathayo 27:54.** Hakuyasema haya kwa sababu ya imani ndani ya Yesu lakini alisema kwa kuyaona matukio ya ajabu yaliotendeka Yesu alipokufa. Bila shaka ushuhuda wa matendo ya Yesu wakati wa kusulibishwa kwake ilithihirisha kwake hakuwa mtu wa kawaida.

## Yesu Mwana wa Mungu

**Waebrania 1:1-3** inaongea kuhusu Yesu Mwana wa Mungu. Maandiko yanafunua mambo manane kuhusu Mwana.

- Mungu anasungumza kupitia Mwana: ***"Mungu ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii"*** **Aya 1.** Tangu Yesu alipokuja, Mungu anasema tu kupitia Mwana. Kwa njia ingine, ni Mwana wa Mungu ambaye ni Mungu anasema. Yesu aliiweka wazi katika **Yohana 14:6** ya kwamba yeye tu ndiye njia ya kufika kwa Baba. Hakuna awezae kuja kwa Baba ila ni kwa njia ya Mwana. Yohana anatangaza katika barua yake, ***"Kila amkanaye Mwana, hanaye Baba; amkiriye Mwana anaye Baba pia"*** **1 Yohana 2:23. {ona pia 1 Yohana 4:15 & 5:12}.**

- Mwana ni mrithi wa yote: ***"Aliyemweka mrithi wa yote"*** **Aya 2.** Katika **Zaburi 2** Mwana anatabiriwa kuwa Mfalme wa Mungu ambaye BWANA ***"Amemweka juu ya Sayuni mlima wangu mtakatifu".*** Kwa Mwana ***"Nitakupa mataifa kuwa urithi wako, na miisho ya dunia kuwa milki yako"*** **Aya 6-8.** Kristo ndiye mrithi wa **Mungu (Warumi 8:17).**

- Aliufanya ulimwengu: ***"Tena kwa yeye aliufanya ulimwengu"*** **aya 2. "Yohana 1:3** ***Vyote vilifanyika kwa huyo; wala pasipo yeye hakikufanyika chochote kilicho fanyika". "kwa kuwa katika yeye vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi, vinavyo onekana na visivyo onekana; ikiwa ni viti vya enzi, au usulutani, au enzi, au mamlaka, vitu vyote viliumbwa kwa jia yake na kwa ajili yake"*** **Wakolosai 1:16.**

- Mwana ni mng'ao wa utukufu wa Mungu: ***"Yeye kwa kuwa ni mng'gao wa utukufu wake"*** **aya 3.** ***"Wakati Mungu alifanyika mtu ndani ya mwanawe, Yesu,"*** maandiko yasema ***"Nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba"*** **Yohana 1:14.** ***"Hakuna mtu aliyemuona Mungu wakati wowote; Mungu mwana pekee aliye katika kifua cha Baba, huyu ndiye aliyemfunua"*** **Yohana 1:18.** ***"Kwakuwa Mungu alisema, nuru itang'aa toka gizani, ndiye aliyeng'aa mioyoni mwetu, atupe nuru ya elimu ya utukufu wa Mungu katika uso wa Yesu Kristo"*** **2 Wakorintho 4:6.**

- Yeye ndiye chapa ya nafsi yake: ***"Na chapa ya nafsi yake"*** **aya 3.** ***"Naye ni mfano wa Mungu asiyeonekana, mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote"*** **Wakolosai 1:15.** Yesu alisema ***"Aliye niona mimi amemwona Baba; basi wewe wasemaje utuonyeshe Baba?"***

**Yohana 14:9b.** ***"Isiwazukie nuru ya injili ya utukufu wake Kristo aliye sura yake Mungu"*** **2 Wakorintho 4:4b.**

- Mwana anavichukua vyote kwa amri ya uweza wake: ***"akivichukua vyote kwa uweza wa amri ya uweza wake"*** **aya 3.** ***"Naye amekuwako kabla ya vitu vyote, na vitu vyote hushikana katika yeye"*** **Wakolosai 1:17.** ***"Kwa neno la Bwana mbingu zilifanyika, na jeshi lake lote kwa pumzi ya kinywa chake"*** **Zaburi 33:6.**

- Yeye mwenyewe alitakasa dhambi zetu: ***"Akiisha kufanya utakaso wa dhambi"*** **aya 3.** ***"Kristo Yesu alikuja ulimwenguni awaokoe wenye dhambi"*** **1 Timotheo 1:15.** ***"Nanyi mnajuwa yakuwa yeye alidhihirishwa, ili aziondoe dhambi; na dhambi haimo ndani yake"*** **1 Yohana 3:5.** ***"Lakini huyu, alipokwisha kutoa kwa ajiri ya dhabihu moja idumuyo…"*** **Waebrani 10:12a.**

- Mwana aliketi katika mkono wa kuume wa Mungu: ***"Aliketi mkono wa kuume wa ukuu huko juu"*** **aya 3.** ***"Lakini huyu …aliketi mkono wa kuume wa Mungu, tangu hapo akingojea hata adui zake wawekwe kuwa chini ya miguu yake"*** **Waebrania 10:12b - 13.** Yesu alifufuliwa na uweza wa nguvu za Mungu ***"Aliotenda katika Kristo alipomfufua katika wafu, akamweka mkono wake wa kuume katika ulimwengu war oho; juu sana kuliko ufalme wote, na nguvu, na usultani, na katika jina litajwalo, wala sii ulimwenguni humu tu, bali katika ujao pia"*** **Waefeso 1:20-21**

## Mungu alidhihirishwa katika mwili

Jia nyepesi yakuelewa Yesu kama Mwana wa Mungu ni kutafakari ushuhuda wa Biblia ya kwamba Mungu alidhihirishwa katika mwili. Mungu hakuwa na mtoto aliyekua afanyike Yesu. La hasha! Mungu alifanyika mwanadamu! ***"Hapo mwanzo kulikuwako neno, naye neno alikuwako kwa Mungu, naye neno alikuwa Mungu"*** **Yohana 1:1.** ***"Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba amejaa neema na kweli"*** **aya 14.** Yesu ni **Neno la Mungu;** Hilo ni mojawapo ya majina yake katika **Ufunuo 19:13.**

Yesu ni Mungu aliyedhihirishwa katika mwili! Sio Mwana wa Mungu kwa kiasiri kwa sababu Mungu ni Roho na Yesu ni **"Mwana wa pekee".** Alipatianwa kwa njia ya Roho Mtakatifu**.** Nikatika ukomavu wake Yesu alidhihirishwa kama Mwana lakini tangia mimba yake aliyekuwa azaliwe alikuwa ajulikane kama Mwana wa Mungu. Yesu hakujulikana kama Mwana wa Mungu mpaka ukamilifu wake, hivyo ni, kutoka wakati wa ubatizo wake katika umri wake wa miaka 30.

Katika **1 Yohana 1:1-3,** Yesu anaelezewa kuwa ***"lile lililokuwako tangu mwanzo"*** na ***"Neno la uzima",*** na hisia tatu zatumika kwa kuelezea: kusikia, ***"Nasi tulilolisikia"*** kuona ***"Tulililoliona kwa macho yetu";*** kugusa ***"Mikono yetu ikalipapasa".*** Yohana anatangaza kwetu ya kwamba ***"Uzima huo ulithihirika"*** **aya 2.** Mungu alidhihirishwa katika mwili na walioshuhudia kwa kuona na kusikia kutazama na kumgusa yeye!

Paulo akiwaandikia **Wafilipi** kumuhusu Yesu Kristo anasema kumuhusu, ***"Ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna mamna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikama nacho; bali alijifanya kuwa hana utukufu akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu; tena alipoonekana ana umbo kama mwanadamu …"*** **(aya**

**2:6-8a).** Mungu alikuja kwa mfano wa wanadamu na akaonekana kwa sura ya mwanadamu! Paulo anaandika ***"Mtu wa kwanza atoka kutoka nchi, ni wa udongo mtu wa pili atoka mbinguni"*** **(1 Wakorintho 15:47).**

### Mungu alijulikana kuwa na haki katika Roho

Mungu, aliyedhihirishwa katika mwili alijulikana kuwa na haki katika Roho. Neno hili *dikaioo* SC# 1344 yamaanisha 'kufanywa haki au bila lawama'. Mungu aliyedhihirishwa katika mwili alishuhudiwa kwa, au akafanywa haki na bila lawama, na Roho Mtakatifu.

Yohana anafunza juu ya kupima roho. Anasema ***"katika hili mwamjua Roho wa Mungu; kila roho ikilio kwamba Yesu Kristo amekuja Katika mwili yatokana na Mungu. Na kila roho isiyo mkili Yesu haitokani na Mungu. Na hii ndio roho ya mpinga Kristo"*** **(1 Yohana 4:2-3a).** Kukili kwa Mungu akidhihirishwa katika mwili ni kufanywa haki ndani ya Roho.

### Roho Mtakatifu anamfanya Yesu haki kama Mwana wa Mungu

- Akiwa kwa mimba. Malaika akizungumzia Mariamu, ***"Roho Mtakatifu atakujilia juu yako, na nguvu zake aliye juu zitakufunika kama kivuli, kwa sababu hiyo hicho kitakacho zaliwa kitaitwa kifakatifu Mwana wa Mungu"*** **Luka 1:35.**

- Katika ubatizo wa Yesu, Roho Mtakatifu alimfanya **mwenye haki** awe **Mwana wa Mungu,** ***"Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini; na tazama, mbingu zikamfunikia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama huwa, akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu ninaye pendezwa naye"*** **Mathayo 3:16-17.**

- Kupitia kufufuka kwake, ***"Yaani, habari za mwanawe, aliyezaliwa katika ukoo wa Daudi kwa jinsi ya mwili, na kudhihirishwa kwa uweza kuwa Mwana wa Mungu, kwa jinsi ya roho wa utakatifu kwa ufufuo wa wafu"*** **Warumi 1:3-4.**

### Alionekana na malaika

Yesu kwa matukio mengi **alionekana na malaika:**

- Malaika alimtangaza Yesu kama Mwana wa Mungu akiwa kwa tumbo ***"Malaika akajibu akamwambia… Hicho kitakacho zaliwa kitaitwa kitakatifu Mwana wa Mungu"*** **Luka 1:35.**

- Malaika walikusanyika wakati wa kuzaliwa kwake, ***"Malaika wa Bwana akawatokea ghafla (wachungaji)…Malaika akawaambia msiogope…maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa, kwa ajili yenu, mwokozi ndiye Kristo Bwana"*** **Luka 2:9-13.**

- Malaika walimhudumia baada ya kujaribiwa katika nyika, ***"Kisha ibilisi akamwacha; na tazama wakaja malaika wakamtumikia"*** **Mathayo 4:11**

- Malaika pia walimhudumia katika bustani ya Gethisemane wakati alijipatiana kwa mapenzi ya baba yake, ***"Malaika kutoka mbinguni akamtokea akamtia nguvu"*** **Luka 22:43**

- Malaika walidhibitisha kifo chake kwa baadhi ya wanawake waliokuja katika kaburi na hawakuupata mwili wa Bwana Yesu Kristo, ***"Ikawa walipokuwa wakifadhaika kwa ajili***

***ya neno hilo, tazama, watu wawili walisimama karibu nao, wamevaa nguo za kumetameta; nao walipo ingiwa na hofu na kuinama kifudifudi hata nchi, hao waliwaambia, kwa nini mnamtafuta aliye hai kati ya wafu?"*** **Luka 24:4-6**

- Malaika walikuwa na wanafunzi kushuhudia kupaa kwa Yesu mbinguni, ***"Walipokuwa wakitazama, akainuliwa, wingu likampokea kutoka machoni pao. Walipokuwa wakikaza macho mbinguni, yeye alipokuwa akienda zake, tazama watu wawili wakasimama karibu nao, wenye nguo nyeupe, wakasema, enyi watu wa Galilaya, mbona mmesimama mkitazama mbinguni? Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomuona akienda zake mbinguni,"*** **Mdo 1:9-11.**

### Akahubiriwa katika Mataifa

Mungu, aliyedhihirishwa katika mwili katika Yesu, amehubiriwa ulimwenguni kati ya Mataifa, Mariko anashuhudia kwamba mitume ***"Nao wale wakatoka, wakahubiri kotekote, Bwana akitenda kazi pamoja nao, na kulithibitisha lile neno kwa ishara zilizofuatana nalo"*** **(Mariko 16:20).** ***"Lakini wale waliotawanyika wakaenda huku na huku wakilihubiri neno"*** **(Mdo 8:4)**

### Akaaminiwa katika ulimwengu

Katika **Mdo 8:35-37** Filipo ***"anamhubiri Yesu"*** kwa toashi wa Kusi. Baada ya kuyasikia mahubiri, kukili kwa huyu mtu kulikuwa, ***"Nimeamini ya kwamba Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu"*** **aya 37.**

### Akachukuliwa juu katika utukufu

Tukio la kushtaabisha la Yesu kuchukuliwa katika utukufu lilishuhudiwa na mitume, ***"Walipokuwa wakitazama, akainuliwa, wingu likampokea kutoka machoni pao"*** **(Mdo 1:9).**

Stephano alikuwa na ufunuo wa Yesu ***Akichukuliwa katika utukufu*** wakati alipaza sauti ***"Tazama! Naona mbingu zimefunguka, na Mwana wa Adamu ameketi mkono wa kuume wa Mungu!"*** **(Mdo 7:56).**

**Kwakushuhudiwa! Na bila shaka, Yesu huyu, aliye Kristo, ni Mungu aliyedhihirishwa katika mwili na akachukuliwa katika utukufu! Huyu Yesu hakika ni Mwana wa Mungu. Amen.**